Jamii

## Tibaigana: Polisi watumie zaidi teknolojia za kisasa

Uk. 28

Biashara

## Mradi wa gesi kuzalisha dizeli, mafuta ya ndege kuanza

Uk. 18

Mzee Tai

## Mkuu wa wilaya hebu acha kubagaza Buza?

Safu Uk. 5

Pambazuko

Toleo Namba 175 | Jumatatu, Julai 27- Agosti 2, 2026


# Mgogoro wa uwekezaji wa $38m Z'bar watishia

- Mwekezaji anadai mradi wa hoteli ya kifahari Pongwe Bay ulizuiwa kinyume cha sheria, ataka suluhu mapema kabla ya kwenda kwenye usuluhishi wa kimataifa

Uk. 6&7

## Nchimbi azua mgongano

"Kama ningeambiwa makamu wa rais waambie Watanzania jambo moja tu, ningesema pambaneni mpate Katiba Mpya. Katiba ambayo ina makubaliano ya wadau wote, Katiba yenye muafaka katika taifa,"



Uk. 9

Habari Uk. 9

## Bodi yadhibiti sukari yenye mchanga

Habari Uk. 23

Tafakuri ya Bagonza

## Umuhimu wa maridhiano ya kweli uko hapa

Safu Uk. 10



## Wachina kutumia Bandari ya Kigoma kubeba madini DRC

Uk. 16



## Tundu Lissu ahenyesha mkuu wa gereza

Habari Uk. 20

# Tahariri

## Wananchi wanataka, serikali ilete Katiba Mpya

KAULI ya Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, kwamba Rais Samia Suluhu Hassan ana dhamira ya dhati ya kuhakikisha Tanzania inapata Katiba Mpya, inapaswa kupokewa kwa matumaini, lakini pia kwa kuhoji maswali ya msingi.

Dkt. Nchimbi mwenyewe amesisitiza kuwa angependa Katiba hiyo ipatikane hata leo, msimamo jumuishi kutoka kwa kilele cha mamlaka ambao unabeba nguvu kubwa ya matamanio ya Watanzania.

Sisi Pambazuko tunaamini kuwa Katiba Mpya ni msingi wa kujenga Tanzania yenye usawa zaidi, uhuru mpana, maendeleo jumuishi na heshima kubwa kwa utu wa kila mwananchi.

Katiba Mpya ndiyo nguzo inayopaswa kuweka mipaka ya madaraka, kuimarisha uwajibikaji, kulinda haki na kuhakikisha hakuna mtu au taasisi inayokuwa juu ya sheria.

Kutokana na msimamo wa viongozi wakuu, ikijumuishwa na matamanio ya Watanzania, Pambazuko tunajenga hoja juu ya swali hili; "kinachosubiriwa ni nini kupata Katiba Mpya?

Zaidi ya hapo, kukamilisha mchakato huo ni ahadi iliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025–2030, hivyo, dhamira ya viongozi, ahadi ya chama na matarajio ya wananchi vinaonekana kuelekea upande mmoja; kwamba Katiba Mpya ipatikane.

Wananchi hawapaswi kuambiwa waende kuvunja mlango ambao funguo zake ziko mikononi mwa wakuu wa serikali na wananchi.

Kauli ya kuwataka "wapambanie" Katiba mpya inaweza kuwa mwito wa ushiriki, lakini haitoshi ikiwa wenye mamlaka ya kuanzisha, kuratibu na kukamilisha mchakato hawajaweka mpango wa wazi.

Sisi tunataka kuona serikali – ambayo ndiyo yenye uwezo wa kuandaa sheria, kutenga fedha, kuweka ratiba, na kuhakikisha mchakato unakuwa huru, shirikishi na wa kuaminika, ikianza kazi haraka.

Tanzania tayari ilitumia fedha, muda na maarifa mengi katika mchakato uliopita, maoni ya wananchi yalikusanywa, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ikafanya kazi na nyaraka muhimu zikaandaliwa, hivyo busara siyo kuanza safari upya, bali kutathmini tulipofikia, kurekebisha kasoro na kusonga mbele kwa uwazi, maridhiano na ushirikishwaji wa pande zote.

Kadiri mchakato unavyoendelea kucheleweshwa, ndivyo hofu inavyozidi kujengeka kwamba huenda kuna ajenda isiyoelezwa ya kuuzuia mchakato wa kupatikana Katiba Mpya.

Hofu hiyo haiwezi kuondolewa kwa hotuba nyingine, bali kwa uamuzi rasmi wenye tarehe, hatua, wajibu na muda wa kukamilisha kazi. Serikali itangaze wazi mchakato utaanza lini, utaendeshwa kwa utaratibu gani na Katiba Mpya inatarajiwa kupatikana lini.

Katiba ya sasa imelifikisha taifa hapa, lakini Watanzania wengi wanaona upungufu unaobana baadhi ya haki, uhuru, uwajibikaji na usawa wa kisiasa.

Pambazuko tunaamini kuwa taifa lenye kujiamini haliogopi kujitazama upya wala kurekebisha misingi yake ili iendane na mahitaji ya kizazi cha sasa na kijacho.

Katiba Mpya haiwezi kuwa mali ya CCM, upinzani, serikali au wanaharakati peke yao, lazima iwe na mwafaka wa kitaifa unaowahusisha wananchi wa makundi yote, Tanzania Bara na Zanzibar.

Mchakato wake ukifanywa kwa haki unaweza kuponya migawanyiko, kurudisha imani katika taasisi na kujenga msingi imara wa amani ya kudumu kwa vizazi vijavyo.

Sisi tunahimiza kuwa wakati wa ahadi zisizo na kalenda – kwa kupatikana kwa Katiba Mpya umepita, na sasa ikiwa viongozi wetu wakuu wanashikilia funguo, wafungue mlango na Watanzania waingie kujiendesha chini ya Katiba Mpya.

## Ziara ya kikazi...



*Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega akisalimiana na Chifu wa Kabila la Wahehe, Adam Abdul Mkwawa. Ulega alikuwa Iringa kwa ziara ya kikazi na kupata fursa ya kukutana na chifu huyo. (Picha na Mpigapicha Maalum).*


## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**



## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na Pale

## 'Vipanga' wa hesabu watuzwa

WAHADHIRI wawili wa hesabu kutoka China wametunukiwa tuzo ya kimataifa ya umahiri wa somo hilo, ikiwa ni mara ya kwanza tuzo hiyo kutolewa kwa wahadhiri wenye asili ya taifa hilo.

Wahadhiri hao kutoka China, Hong Wang na Yu Deng wameongoza katika tuzo hiyo, wakifuatiwa na John Pardon kutoka Marekani na Jacon Tsimerman wa Canada.

Wote wametunukiwa tuzo hiyo baada ya kutafuta suluhisho la kihesabu katika masuala yaliyotatiza wanahisabati kwa karibu karne nzima, kupitia tuzo hiyo inayolinganishwa na Tuzo ya Nobel kwa wataalamu wa hisabati.

Tuzo hiyo inatolewa kwa wanataaluma wa hisabati bila kutumika kwa msaada wa Akili Unde (AI).

## Washirika wa Trump kukwama

NCHI 60 zinazojihusisha na biashara na Marekani zinakabiliwa na vikwazo vipya vya kibiashara, baada ya nchi hiyo kuweka viwango vipya vya ushuru tangu Rais Donald Trump alipoingia madarakani mwaka jana.

Washirikia hao wa karibu wa Marekani, ikiwemo Uingereza, China na Umoja wa Ulaya, sasa watalazimika kukabiliana na ongezeko la asilimia 10 hadi 12 la ushuru kwa bishaa zake zinazoingizwa Marekani.

Ushuru huo unatarajiwa kuanza baada ya kumalizika kwa muda maalumu wa mpito katika masuala ya kodi ya bidhaa Ijumaa iliyopita.



Mwanzoni mwa mwaka huu, Mahakama ya Rufaa ya Juu ya Marekani ilitoa uamuzi ulioeleza kuwa ushuru unaoongezwa na mamlaka dhidi ya bidhaa za nje umekuwa hauzingatii sheria.

## Afrika na Katibu Mkuu UN

HUENDA AFRIKA ikatoa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) baada ya kupita miaka 20 tangu kuondoka kwa Kofi Annan.

Annan ambaye ni raia wa Ghana alikuwa Mwafrika wa pili kushika nafasi hiyo.

Kwa sasa, anayepigiwa chapuo kushika nafasi hiyo ni aliyekuwa Rais wa Senegal, Macky Sall ambaye huenda akapambanishwa na wengine watano wanaowania nafasi hiyo kutoka Amerika ya Kusini na Carribean.

Sall anaingia katika kinyang'anyiro hicho akiwa Mwafrika pekee, akipambana kuwa mrithi wa katibu mkuu wa sasa, Antonio Gutteres ambaye muda wake unatarajiwa kumalizika Desemba 31 mwaka huu. Mwafrika wa kwanza kushika wadhifa huo alikuwa Butros Ghali kutoka Misri (1992-1996). Annan alikuwa na dhamana hiyo 1997 hadi -2006.



## Traore hataki kabisa wazushi

RAIS wa Burkina Faso, Kapteni Ibrahim Traoré, ametoa onyo kali akitaka kuheshimiwa kwa utawala wake, wakati akijaribu kuzima uvumi wa kuwepo kwa mzozo wa madaraka ndani ya serikali.

Traore amesema nchi hiyo inaweza kuwa na kiongozi mmoja pekee, bila kuangalia nani wengine wapo.

Kauli hiyo inafuatia uvumi ulioibuka baada ya maofisa wawili wa ngazi za juu wenye ushawishi wa hali ya juu nchini humo kutoonekana hadharani; Oumarou Yabré na Farouk Azaria Sorgho.

"Haiwezekani kuwa na makapteni wawili katika meli moja," Traoré aliwaambia viongozi wa jamii mjini Ouahigouya, kaskazini mwa Burkina Faso, Alhamisi iliyopita akisema kuwa uongozi wake haujaribiwi.

Na Mzee TAI

# Mkuu wa wilaya hebu acha kubagaza Buza?

MKUU wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda, ameikamia Buza, sijui amegundua nini hata kuamua kuzodoa eneo linaloinukia kwa maendeleo ya haraka, baada ya wakazi wake kuhamia huko wakitokea maeneo mengine.

Kwa maelezo yake, anaeleza kuwa kuwekwa kwa mnada wa magari ya kifahari; Lamborghini, Lexus na Mercedes-Benz, katika eneo hilo kunaweza kuwa dalili ya matokeo ya "mchezo mchafu wa wauza dawa za kulevya" au watu wengine wanaojihusisha na biashara haramu.

Kauli hii ni nzito, bila shaka. Ni aina ya kauli inayoweza kufanya hata gari lililoegeshwa kwa heshima lianze kutetemeka vioo.

Mimi ambaye nimehamia Buza majuzi, nimebaki kukunja uso na kuhesabu maswali, najiuliza; hivi kosa la magari hayo ni kuwa Buza, au ni bei zake, majina yake na kung'aa kwake?

Kama yangepangwa Masaki, Oysterbay au Upanga, yangeonekana kuwa ishara ya uwekezaji, lakini Buza yakawa ushahidi wa shaka? Kumbe hata magari yanaweza kuhukumiwa kwa anwani janami!

Hakuna anayepinga mamlaka kuchunguza uhalifu, hasa huu wa biashara ya dawa za kulevya, utakatishaji fedha na mapato yasiyoelezeka. Haya ni maovu yanayopaswa kufuatiliwa bila huruma.

Hata hivyo, uchunguzi wa maana haupaswi kuanza na kumalizika kwenye uzio wa mnada pekee, unapaswa kufuatilia nyaraka za uingizaji, ushuru uliolipwa, taarifa za benki, umiliki halisi wa magari, historia ya ununuzi na chanzo cha fedha. Hapo ndipo shaka hubadilishwa kuwa ushahidi, au mfanyabiashara huondolewa kwenye kivuli cha tuhuma.

Mini nashangaa zaidi kwamba magari haya yametoka Japan, Ulaya au kwingineko, yakasafirishwa maelfu ya kilometa, yakapitia bandari, forodha, mamlaka za mapato, benki, wakala wa usafirishaji na usajili. Katika safari hiyo ndefu, hakuna aliyeyaona? Hakuna aliyejiuliza thamani yake, mwenye kuyamiliki au fedha zilizoyaleta? Kwa nini swali kubwa linaanza tu baada ya magari kufika Buza na kusubiri wanunuzi?

Ni vyema watu wenye mamlaka wakajenga utamaduni wa kuchuja maneno, hasa wanapokuwa kwenye majukwaa, kauli ya kiongozi inaweza kuweka tahadhari, lakini inaweza kuharibu biashara, kutisha wanunuzi na kuchafua jina la eneo kabla uchunguzi haujathibitisha chochote.

Sisi wakazi wa Buza siyo watazamaji wa uhalifu; ni wananchi wanaofanya kazi, kulipa kodi na kutafuta maendeleo kama wenzao wa maeneo mengine.

Ikiwa kuwa na bidhaa kunazua maswali, basi maswali hayo yaulizwe kwa utaratibu unaofanana kila mahali, tusije tukawa na sheria inayovaa tai Masaki, lakini ikifika Buza inavaa sare za upekuzi.

Haki huonekana kuwa haki pale inapowapima wote kwa mizani moja, hadharani bila ubaguzi wala dharau.

Ikiwa yapo makosa, wahusika wachunguzwe na sheria ichukue mkondo wake, lakini tusigeuze eneo la Buza kuwa hati ya mashaka, wala gari la kifahari kuwa hukumu inayotembea bila ushahidi.

Mimi kwa uzee wangu naamini kuwa uhalifu hauna kata wala kijiji, na uadilifu pia haupaswi kuwa na ramani ya vitongoji.

Pengine mkuu huyo wa wilaya ametuma tahadhari muhimu. Hata hivyo, tahadhari hiyo itakuwa na maana zaidi ikiwa itafungua uchunguzi wa mnyororo mzima, badala ya kuangaza maegesho pekee, tena yakitajwa yale ya Buza na maeneo mengine ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam.

Akili yangu ya uzee, kama Lamborghini limevuka bahari bila kuulizwa chochote, halipaswi kubeba uhalifu kwa sababu tu limefika Buza, vinginevyo, kesho hata mwenye kuvaa suti nzuri maeneo ya mjini ataombwa kueleza amewezaje kuwa mtanashati wakati anaishi Buza?

## Habari Kuu

# Mgogoro wa uwekezaji wa $38m Z'bar watishia



*Waziri wa Mambo ya Nje wa Tanzania, Mahmoud Thabit Kombo*

**Na Mwandishi WETU**

MGOGORO wa kisheria unaohusisha mwekezaji kutoka Uingereza na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umeibua mjadala kuhusu ulinzi wa uwekezaji wa kigeni, uwazi wa taratibu za kiutawala na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya uwekezaji.

Mwekezaji huyo, kupitia kampuni ya Opulent (Pongwe Zanzibar) Limited, anadai kuwa uwekezaji wake wa takribani dola za Marekani milioni 38 katika eneo la Pongwe, Zanzibar, umeathiriwa na hatua za mamlaka za serikali ambazo anazielezea kuwa hazikufuata taratibu za kisheria, hivyo kukiuka wajibu wa Tanzania chini ya mkataba wa uwekezaji kati ya Uingereza na Tanzania (UK-Tanzania Bilateral Investment Treaty - BIT).

Mradi huo, ulioanzishwa mwaka 2016, ulikuwa unalenga kujenga kituo cha utalii cha kiwango cha kimataifa chenye hoteli yenye chapa ya Marriott, majengo 60 ya makazi, pamoja na majengo 38 ya kifahari ya malazi.

Nyaraka za mwekezaji ambazo Pambazuko imeziona zinaonyesha kuwa mradi huo ulitarajiwa kuzalisha zaidi ya ajira 300 za moja kwa moja kwa wakazi wa Zanzibar.

Hata hivyo, nyaraka nyingine zinaonyesha kuwa kile kilichoanza kama mradi mkubwa wa uwekezaji katika sekta ya utalii kimegeuka kuwa mzozo wa kisheria unaoweza kufikishwa katika Mahakama ya Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji ya Kimataifa (ICSID) jijini Washington DC, Marekani, iwapo hakutapatikana suluhu kati ya pande hizo.

Katika hatua ya awali mwekezaji huyo ameemuandikia Mwanasheria Mkuu wa Tanzania, Hamza Johari, akitoa malalamiko yake na kuitaka serikali kuchukua hatua za kulinda uwekezaji wake kama inavyoelekezwa kwenye BIT.

Mwekezaji: Tumetekeleza wajibu wetu

Katika malalamiko yake ya kisheria kwa Mwanasheria Mkuu Aprili mwaka huu, Opulent inasema imekuwa ikitimiza wajibu wake wote wa kisheria na kifedha tangu ilipopata eneo hilo la uwekezaji.

Barua hiyo ya malalamiko imenakiliwa pia kwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Tanzania, Mahmoud Thabit Kombo, Wakili wa Serikali, Ally Possi, Waziri wa Ardhi wa Zanzibar, ZIPA na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

Mlolongo wa nyaraka unaonyesha kuwa kampuni hiyo imekuwa ikilipa kodi ya pango la ardhi ya takribani dola 26,000 kwa mwaka pamoja na ada nyingine za kisheria, huku malipo hayo yakidaiwa kuwa yamefanyika tangu mwekezaji alipopewa ardhi hadi Februari 2027.

Aidha, mwekezaji huyo anasema alipata vibali mbalimbali kutoka mamlaka husika Zanzibar, ikiwemo Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), ambayo ilipitia na kuidhinisha mabadiliko ya muundo wa mradi mwaka 2023 kutoka mradi wa hoteli pekee kwenda mradi mchanganyiko wa hoteli na makazi.

Inaendelea Uk. 7

# Mgogoro wa uwekezaji wa $38m Z'bar



Inatoka Uk. 6

Kwa mujibu wa nyaraka za kisheria zilizowasilishwa na mwekezaji huyo kwa Mwanasheria Mkuu na Pambazuko kuona nakala zake, ZIPA pia iliruhusu kuongezwa kwa muda wa utekelezaji wa mradi hadi Januari 2026 na baadaye kuidhinisha mabadiliko ya muundo wa kampuni mwaka 2025.

Mwekezaji anasema pia aliendelea kuwa katika eneo la mradi, akijenga ukuta wa uzio, kufanya maandalizi ya awali ya ujenzi na kupata vibali vya mazingira.

Kwa mtazamo wake, hatua hizo zilionyesha kuwa mradi ulikuwa unaendelea kwa mujibu wa taratibu na kwamba hakukuwa na sababu ya kisheria ya kufuta haki zake juu ya eneo hilo.

### Mzozo wa hati ya ardhi

Kwa mujibu wa nyaraka hizo, chanzo kikuu cha mgogoro huo kinahusishwa na hati ya upangaji wa ardhi ambayo kampuni hiyo iliitumia kama dhamana kupata mkopo kutoka Benki ya Baroda.

Kwa mujibu wa malalamiko hayo, wakati benki hiyo ilipokuwa katika mchakato wa marekebisho ya mikopo na taratibu za kifedha, hati halisi ya upangaji ilipotea na benki ikaomba kupatiwa nakala nyingine kutoka Ofisi ya Usajili wa Ardhi Zanzibar.

Hata hivyo, badala ya kupatiwa nakala mbadala ya hati hiyo kama utaratibu wa kawaida, mawakili wa benki hiyo walidaiwa kupewa taarifa kwa njia ya mazungumzo kwamba hati hiyo ilikuwa tayari imefutwa, kubatilishwa au kutolewa kwa mtu mwingine.

Mwekezaji anadai kushangazwa na hatua hiyo kwani kabla ya hapo hakuwahi kupokea taarifa rasmi ya kusitishwa kwa mkataba wa upangaji wa ardhi, wala hakuwahi kupewa amri ya maandishi yenye saini kutoka mamlaka husika ikieleza sababu za hatua hiyo.

Pia anadai katika sakata hilo lote mamlaka za serikali zinatumia nakala ya barua ya kusitisha mkataba ambayo haina na saini rasmi.

Mwekezaji huyo anashangazwa na hatua ya mamlaka kukataa kutoa nyaraka kamili zinazoeleza uhalali wa uamuzi huo wa kufuta hati hiyo iliyotolewa kihalali.

Kwa mujibu wa nyaraka za mwekezaji huyo, hali hiyo ilisababisha kutokuwa na uhakika wa kisheria kuhusu umiliki wa haki ya matumizi ya eneo hilo, jambo lililosababisha kusimama kwa maandalizi ya utekelezaji wa mradi.

### Madai ya kutokuwepo kwa uwazi

Hoja kubwa ya Opulent ni kwamba kulikuwa na mgongano wa hatua zilizochukuliwa na taasisi mbalimbali za serikali kuhusiana na suala hilo.

Wakati upande wa ardhi mwekezaji huyo anadai kuwa mkataba wa upangaji ulikuwa umefutwa kwa sababu ya kutotekelezwa kwa maendeleo ya mradi, huku taasisi nyingine za serikali ziliendelea kumtambua kama mwekezaji halali.

Mfano uliotolewa ni kwamba Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) iliendelea kuiletea ankara za madai ya malipo ya kodi ya pango la ardhi, huku ZIPA ikiendelea kutoa nyaraka za kuongeza muda wa utekelezaji wa mradi.

Kwa mtazamo wa mwekezaji, hali hiyo ilizua mazingira ya kutokuwa na uhakika wa kisheria na kukiuka matarajio halali ambayo wawekezaji wanapaswa kupata kutoka kwa serikali inayotaka kuvutia mitaji ya kimataifa.

Inaendelea Uk. 8

# Mgogoro wa uwekezaji...

Inatoka Uk. 7

**Mkataba wa uwekezaji wa kimataifa**

Kupitia kampuni ya mawakili ya Fladgate LLP, mwekezaji huyo aliwasilisha taarifa rasmi ya mgogoro kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Tanzania Aprili 17, 2026.

Katika taarifa hiyo, mwekezaji anadai kuwa hatua zilizochukuliwa na mamlaka za Zanzibar zinahusishwa moja kwa moja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

Malalamiko hayo yanahusisha madai ya ukiukwaji wa vipengele kadhaa vya Mkataba wa Uwekezaji kati ya Uingereza na Tanzania.

Kwanza, mwekezaji anadai Tanzania imekiuka kifungu kinachohusu haki na usawa kwa wawekezaji (Fair and Equitable Treatment) kwa kushindwa kuweka uwazi, kufanya uamuzi usiotabirika na kuchukua hatua bila utaratibu unaostahili. Pili, mwekezaji anadai hatua za kufuta au kugawa upya haki ya matumizi ya ardhi bila yeye kupewa taarifa rasmi, bila mchakato wa kisheria na bila fidia stahiki zinaweza kutafsiriwa kama unyakuzi haramu wa uwekezaji (unlawful expropriation) chini ya sheria za kimataifa.

Tatu, mwekezaji anadai kuzuiwa kwa mchakato wa kupata nakala ya hati ya ardhi kumeathiri uwezo wake wa kupata fedha na kuendeleza mradi, jambo analodai linaathiri haki yake ya kufaidika na uwekezaji wake.

**Akimbilia usuluhishi wa kimataifa**

Baada ya kuwasilisha taarifa ya mgogoro, pande hizo zimeingia katika kipindi kinachojulikana kisheria kama cooling-off period, ambapo wahusika hupewa muda wa kutafuta suluhu kabla ya kuanza kesi rasmi ya kimataifa.

Mwekezaji amesema yuko tayari kushiriki mazungumzo ya kibiashara na serikali ili kupata suluhu ya mgogoro huo.

Hata hivyo, ameweka wazi kuwa iwapo hakutakuwa na ufafanuzi wa kisheria au hatua za kurekebisha hali hiyo, anaweza kuanzisha mchakato wa usuluhishi katika ICSID.

Hatua hiyo inaweza kuiweka Tanzania katika mazingira ya kutakiwa kulipa fidia ya mamilioni ya dola iwapo chombo hicho kitaamua kuwa nchi imekiuka wajibu wake wa kimataifa.

**Athari kwa mazingira ya uwekezaji**

Mgogoro huu unakuja wakati Tanzania ikiendelea kutangaza sera za kuvutia uwekezaji wa ndani na nje, hususan katika sekta za utalii, nishati, madini na viwanda.

Kwa nchi zinazoshindania mitaji ya kimataifa, wataalamu wa masuala ya uwekezaji wanaeleza kuwa uhakika wa sheria, uwazi wa taratibu na ulinzi wa haki za wawekezaji ni miongoni mwa vigezo muhimu vinavyozingatiwa na wawekezaji wakubwa.

## Stendi ya Magufuli...






*Majengo ya Stendi Kuu ya Mabasi ya Chato yakiwa yamefungwa kutokana na kukosa wateja wa kufanyia biashara ambapo miundombinu yake imeanza kuchakaa kama ilivyokutwa na kamera ya Pambazuko juzi.*

# Dkt Nchimbi azua mgongano

**Na Mwandishi WETU**




KAULI ya Makamu wa Rais, Dkt. Emmanuel Nchimbi, kwamba Watanzania waipambanie Katiba Mpya, imeacha mlolongo wa maswali, mshangao na imani mchanganyiko.

Kwa namna kauli hiyo inavyojadiliwa, ni dhahiri kuwa imeacha pia mvurugano miongoni mwa wanasiasa, wanazuoni na wachambuzi kuhusu mwenendo wa uongozi na utawala hapa nchini.

Kauli hiyo inaonekana kuacha hewani baadhi ya mambo na kuweka ombwe ambalo limeendelea kutoa nafasi kwa kila mtu kutafsiri awezavyo kuhusu nini alimaanisha msaidizi huyo namba mbili wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa upande mwingine, kauli hiyo tata ya Dkt. Nchimbi imeleta mgawanyiko wa fikra, mitazamo na tafakari juu ya malengo halisi ya kauli hiyo huku wengine wakiielezea na kuichukua kwa tahadhari kubwa.

Maswali yaliyoibuka miongoni mwa mengi ikiwamo; kwanini Watanzania waipambanie Katiba Mpya wakati Rais Samia, siyo tu kuwa ana utashi wa kufanya hivyo, bali aliwahakikishia Watanzania kuwa kuandika Katiba Mpya ni moja ya mambo ambayo angeyatekeleza ndani ya siku 100 za uongozi wake.

Labda, kusuasua kwa mchakato huo kuliwafanya baadhi ya watu kukata tamaa na kuichukulia kama sehemu ya ahadi zinazotolewa na viongozi ambazo hazina dhamira ya utekelezaji nyuma yake.

Ndiyo maana baadhi ya watu wanahoji dhima hasa ya kauli ya Dkt. Nchimbi kuwataka wananchi waipambanie Katiba Mpya kwani hakuna ambacho kipo nje ya uwezo wa serikali kufanikisha kupatikana kwake.

Dkt. Nchimbi – kwa kauli yake hiyo, ameibua sintofahamu hiyo wakati wa Mkutano Mkuu wa 15 wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Julai 24, 2026 jijini Dar es Salaam.

Akihutubia mkutano huo, Dkt. Nchimbi alieleza kuwa jambo kubwa ambalo Watanzania wanapaswa kulipa kipaumbele kwa sasa ni kupatikana kwa Katiba Mpya, akisema ndiyo sheria mama inayoweza kubeba na kusimamia masuala mengine yote ya utawala bora nchini.

“Kama ningeambiwa makamu wa rais waambie Watanzania jambo moja tu, ningesema pambaneni mpate Katiba Mpya. Katiba ambayo ina makubaliano ya wadau wote, Katiba yenye muafaka katika taifa,” alisema.

Katika hilo alisisitiza kuwa hata Rais Samia mwenyewe anaitaka Katiba Mpya na anatamani ipatikane kabla ya uchaguzi mkuu ujao na ndio maana suala hilo likawekwa kwenye Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) anachokiongoza.

**Wadau waibuka**

Kauli hiyo imewaibua wadau mbalimbali wakihoji kuna sababu gani ya Watanzania kupambania Katiba mpya wakati rais, ambaye ndiye kiongozi mkuu wa nchi ana utashi huo?

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe, Dkt. Benson Bagonza, ameibua maswali kadhaa huku akiwataka Watanzania kuendeleza jitihada za kudai mabadiliko ya Katiba katika taifa lao.

Inaendelea Uk. 14

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Umuhimu wa maridhiano ya kweli uko hapa

NAKARIBIA kumaliza mwaka mmoja nikiwa mwalimu wa chuo kikuu. Kimsingi, kila askofu ni mwalimu, lakini siyo kila mwalimu ni askofu.

Isivyokuwa bahati, nina vyote! Tangu Septemba 2025 nafundisha somo la Political Philosopy (filosifia ya siasa) kwa wanafunzi wanaosoma sayansi ya siasa.

Hapa mezani kwangu, nina nyaraka za maridhiano ya nchi za Afrika Kusini, Rwanda, Kenya, Sierra Leone, Gambia na Cyprus.

Kila nchi ina mazingira yake, lakini maridhiano ni suala linalohitajika endapo "jambo kubwa lisilo la kawaida" limetokea na kuigawa nchi kwa vitendo vyenye sura ya jinai kubwa ambavyo hata vikinyamaziwa, vitakwamisha ustawi wa taifa husika.

Ziko faida nne za maridhiano bila kujali nchi iko wapi na ina historia gani.

Njia ya kwanza, ni njia ya kuanza upya baada ya kukosea. Unakiri na kuomba kuanza upya.

Pili, ni kujifunza "kushindwa" na sauti inayodai uwajibikaji wa kijamii. Unakubali kushindwa hata kama unaamini umeshinda.

Tatu, ni njia kuzuia "ufukuaji wa makaburi" hapo baadaye. Hili ni muhimu sana hata ndani ya vyama na serikali tawala kuliko vyama pinzani. Bila hatua hii, watu hugeuza historia kuwa agenda ya kisiasa.

Nne, ni njia ya kuwatoa kifungoni watawala na kuwarejeshea mamlaka ya kimaadili (Moral authority). Hii ni kuweka silaha chini na kuongoza kwa ushawishi. Wananchi walionuna wana nguvu kuliko maandamano.

Jambo la muhimu zaidi ni kuhakikisha katika kufikia maridhiano, hakuna mtu anayeachwa.

Nyaraka zote nilizonazo zinasisitiza ulazima na umuhimu wa maridhiano na kwamba, "Usimwache nje mtu au kundi lolote lenye ushawishi, ambalo linaweza kurudisha nyuma mapatano yote yaliyofikiwa wakati limeachwa nje".

Ushawishi una nguvu kuliko silaha. Mwenye silaha hujaa kiburi wakati mwenye kushawishi hutumia akili na hekima.

Mjaluo mmoja ameniambia kuwa kuchelewesha maridhiano ya kweli ni sawa na kuchambia maji ya pilipili.

Akaongeza, ujanja ujanja hautakiwi katika maridhiano.

Sijui amejuaje wakati Wajaluo wakimaliza huwa wanaenda ziwani kuogelea na kumaliza "shughuli" zao humohumo ndani ya maji.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***





Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

# Ulinzi wa kitaaluma kwa wahadhiri utafakariwe

NIMEJIKUTA nikijiuliza iwapo mwalimu au mhadhiri wa somo la siasa, anaweza kufundisha bila hofu kufuatia taarifa za mhadhiri kushtakiwa kwa kosa la ugaidi.

Taarifa za kukamatwa tena na kufunguliwa mashtaka ya ugaidi kwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Melkisedeck Kitunzi Kaijage, anayefundisha somo la serikali na siasa za Tanzania; uhuru hadi sasa, zimeibua maswali mengi na kukuza mijadala hapa nchini na hata nje ya nchi.

Tunakumbuka ni mhadhiri huyu huyu aliwahi kukamatwa akidaiwa kuhamasisha maandamano ya Oktoba 29 mwaka 2025.

Madai hayo yalitokana na mafundisho yake akiwa darasani na aliachiwa baada ya hapo.

Akiwa anaendelea na kazi yake hiyo amekamatwa tena na safari hii akituhumiwa kuhamasisha maandamano ya Julai 7 ambayo hatukuyaona.

Mawakili na wahadhiri wenzake walikuwa wakifuatilia upatikanaji wa dhamana ili aendelee na hiyo kesi aliyokamatiwa wakataarifiwa kuwa shtaka limebadilika na anashtakiwa kwa kesi ya ugaidi ambayo haina dhamana.

Bila kuingia katika undani wa kesi iliyoko mahakamani dhidi yake ambayo inapaswa kuzingatia ushahidi utakaotolewa na kwa mujibu wa sheria na haki, tunayo sababu kulitazama tukio hili kwa upana wake kuhusu walimu wa siasa wanavyoweza kufundisha bila hofu katika hali kama hii.

Ninavyoelewa mimi lengo la somo la siasa ambalo liko katika mitaala ya vyuo na hata shule ni kuwawezesha wanafunzi kuelewa mifumo ya utawala, demokrasia, katiba, sheria, haki za binadamu na hata migogoro ya kisiasa na inavyoweza kujenga au kupoteza utulivu.

Katika kufundisha kwa ufanisi inamlazimu mwalimu kuelezea hoja mbalimbali na hata kudadavua hoja tata na zinazokinzana.

Mwalimu anaweza kutumia mifano kisa mkasa na hata hali halisi za wakati huo nchini, na hata nchi nyingine zozote duniani ili kutoa upeo wa hali halisi katika somo analolifundisha.

Hapo ndipo umuhimu wa uhuru wa kitaaluma unaibuka.

Vyuo Vikuu ni sehemu ambayo elimu yake ni ya upeo zaidi ni mahali pa kuuliza maswali magumu, kuchambua mawazo yanayotofautiana, kujaribu kutafuta ukweli kwa kujadili ushahidi wa kitaaluma, kuweza kupembua mambo kwa uwazi bila kuwa na mashaka au wasiwasi.

Ikifikia mahali wahadhiri wakawa na hofu katika njia wanazotumia kufafanua hoja mbalimbali kwa kudhani yale watakayoyafundisha au kuyafafanua huenda yakatafsiriwa vinginevyo, itakuwa ni hatari ya kupoteza uwezo wa kuwajenga wanafunzi wanaoweza kufikiri kwa kiwango stahiki.

Mara nyingi wapo watu ambao huwa hawaelewi hoja hizi zinapotafakariwa wakidhani kuwa nafasi ya dola ya kulinda usalama wa taifa inaingiliwa.

Wapo wanaodhani kipo kipimo cha mtu kuweza kujieleza na wapo wasiofahamu kabisa suala la uhuru wa kitaaluma walionao wanataaluma wawapo katika kazi hizo za kitaaluma.

Tunachoangalia hapa ni kuwa hata pale masuala ya kiusalama yanavyoangaliwa pawepo na ufahamu wa kina wa ulinzi wa uhuru wa kufundisha, kujifunza na hata kufanya utafiti.

Tunaweza kujenga jamii yenye usalama wa kudumu iwapo tutaulinda usalama bila kuzuia fursa katika kupokea maarifa na uwepo wa fikra huru.

Ninavyozidi kutafakari kwa kumtazama huyu mhadhiri anayechomolewa kutoka darasani na kufikishwa kizimbani kwa yale anayoyafundisha.

Najiuliza hivi tunategemea kujenga taifa lililo na viongozi na watendaji wenye uwezo wa kufikiri na kujenga hoja zitakazoleta mabadiliko chanya ya kimaendeleo nchini, iwapo walimu wao watafundisha kwa hofu.

Taifa linalojiamini haliwezi kuhofia maarifa.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

# Olengurumwa: Serikali ithamini asasi za kiraia




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo (wapili kushoto) akizindua mpango wa ruzuku kuhamasisha haki za binadamu wakati wa Mkutano Mkuu wa 15 wa THRDC uliofanyika Julai 24, 2026 jijini Dar es Salaam. Wa pili kulia ni Mratibu THRDC, Wakili Onesmo Olengurumwa. (Picha na THRDC)*

**Na Mwandishi WETU**

MRATIBU wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Wakili Onesmo Olengurumwa, ameiomba serikali kuendelea kuimarisha mazingira wezeshi kwa asasi za kiraia.

Katika hilo amehimiza kuanzishwa kwa mifumo endelevu ya uhamasishaji wa rasilimali za ndani kufuatia kupungua kwa ufadhili kutoka kwa wahisani wa kimataifa.

Olengurumwa alitoa kauli hiyo mbele ya Makamu wa Rais, Dkt. Emmanuel Nchimbi, wakati wa Mkutano Mkuu wa 15 wa THRDC uliofanyika Julai 24, 2026 jijini Dar es Salaam.

"Kufikiria upya ufadhili wa miradi ya haki za binadamu kupitia ubunifu, uwekezaji na uhamasishaji wa rasilimali za ndani, inalenga kutafuta suluhisho la changamoto ya kupungua kwa ruzuku za nje zilizokuwa zikisaidia shughuli za haki za binadamu," amesema Olengurumwa.

Amesema THRDC yenye zaidi ya wanachama 350 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, imeanzisha mpango unaolenga kukusanya rasilimali kutoka sekta binafsi, wahisani wa ndani na nje.

Amesema lengo ni kusaidia asasi ndogo za kiraia na kuongeza uwezo wa sekta hiyo kujitegemea kifedha.

"Serikali kuunga mkono ujenzi wa Watetezi House katika mji wa serikali Mtumba, Dodoma kuboresha mfumo wa uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR).

"Kuweka mazingira rafiki ya kodi kwa asasi za kiraia na kuharakisha kupitishwa kwa sera ya taifa ya kuwatambua na kuwalinda watetezi wa haki za binadamu," amesema.

Olengurumwa amesisitiza umuhimu wa kuimarisha maridhiano ya kitaifa, kuendeleza mchakato wa Katiba mpya na kuridhia mikataba ya kimataifa inayolenga kupinga mateso na kutoweshwa kwa watu kwa nguvu.

Amesema asasi za kiraia zimekuwa washirika muhimu wa serikali katika sekta za afya, elimu, kilimo, mazingira, msaada wa kisheria na utawala bora huku zikichangia ajira, mapato ya kodi na maendeleo ya jamii.

Akasisitiza kuwa ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi na asasi za kiraia ni nguzo muhimu katika kufanikisha Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na kujenga taifa lenye haki, amani na maendeleo endelevu.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya THRDC, Pili Mtambalike, alisema maridhiano ya kitaifa, mshikamano na umoja ni ushindi wa kujenga taifa lenye amani na maendeleo endelevu.

Alisema maendeleo ya kweli hayawezi kupatikana bila kuwepo kwa mazingira yanayolinda haki za binadamu na yanayowapa wananchi nafasi ya kushiriki katika maamuzi yanayowahusu.

Wakati huohuo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, aliipongeza THRDC kwa kuanzisha mpango wa ruzuku kuhamasisha haki za binadamu (Human Rights Grant Project), akisema utakuwa chachu ya kuongeza upatikanaji wa rasilimali fedha.

Profesa Kitila alitoa pongezi hizo wakati akizindua mpango huo huku akichangia Shilingi milioni moja kuunga mkono utekelezaji wake.

# THRDC: Ulinzi haki za watoto ni uwekezaji wa maendeleo

**Na Mwandishi WETU**

MRATIBU wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, amesema uwekezaji kwa watoto ni msingi wa kujenga taifa lenye maendeleo endelevu.

Amesema hayo wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa watetezi wa haki za watoto ngazi ya jamii yaliyofanyika jijini Dar es Salaam Julai 23, 2026.

Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo watetezi katika ufuatiliaji, uandishi na utoaji wa taarifa za ukiukwaji wa haki za watoto nchini.

"Ili taifa lifikie maendeleo tunayoyataka, ni lazima tuwekeze kwa watoto, taifa lisilowekeza kwa watoto ni taifa lililokufa kwa sababu watoto ndio msingi wa kizazi kijacho," amesema.

Olengurumwa amesema mtoto anapaswa kulindwa tangu akiwa mdogo, ili akue katika mazingira salama na aweze kuwa raia mwenye uwezo wa kujitegemea na kuchangia maendeleo ya jamii na taifa.

Akasisitiza umuhimu wa watoto kupata elimu bora inayojumuisha haki za binadamu, maadili na uwajibikaji.

Amewataka watetezi wa haki za watoto kuendelea kujifunza kuhusu sheria, sera na mifumo ya ulinzi wa mtoto inayobadilika mara kwa mara.

Akitoa mada katika mafunzo hayo, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)-Shule ya Sheria, Dkt. Veronica Buchumi, amewataka watetezi hao kujenga uelewa wa kina kuhusu sheria mbalimbali zinazolinda haki za mtoto.

Dkt. Buchumi amesema watetezi hao wakiwa na uelewa huo itawawezesha kuhushughulikia ipasavyo masuala ya ukiukwaji wa haki hizo kwa kuzingatia misingi ya kisheria.

Amesema uelewa wa sheria zinazohusu ulinzi wa mtoto ni nyenzo muhimu kwa watetezi wa haki za binadamu.

"Hii itawasaidia kutambua haki za watoto, kufuatilia ukiukwaji wake na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria," amesema.

Akatoa mwito kwa jamii kutambua kuwa ulinzi wa haki za watoto ni jukumu la kila mwananchi na si la serikali au taasisi pekee.



*Makamu wa Rais Dkt. Emmanuel Nchimbi akimsikiliza Mratibu wa THRDC, Wakili Onesmo Olengurumwa wakati wa Mkutano Mkuu wa 15 wa THRDC uliofanyika Julai 24, 2026 jijini Dar es Salaam.*

"Ushiriki wa jamii katika kutambua kuripoti na kuzuia vitendo vya ukiukwaji wa haki za watoto ni muhimu katika kuhakikisha watoto wanakua katika salama na yenye kuheshimu haki zao.

Kwa upande wake, Mhadhiri kutoka Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Zachayo Shigongo, amesema masuala ya haki za mtoto yanagusa maeneo yote ya maisha ya mwanadamu kijamii, kiuchumi na kisiasa.

"Kwa sababu hiyo, utetezi wa haki za watoto haupaswi kuwa jukumu la mtu mmoja au taasisi moja, bali unahitaji ushirikiano wa wadau wote, taaluma mbalimbali, na serikali," amesema Shigongo.

Naye Mkurugenzi wa Miradi na Uendeshaji wa THRDC, Halima Sonda amewataka watetezi hao kuweka vipaumbele katika shughuli za uchechemuzi kwa kuelekeza nguvu kwenye masuala machache yenye athari kubwa.

"Licha ya kuwepo kwa changamoto nyingi zinazowakabili watoto, ni muhimu watetezi kuchagua ajenda moja au chache zenye kipaumbele…"

"Wakifanya hivyo itasaidia kufuatiliwa kwa umakini na kupata matokeo kwa haraka. Pia wanapaswa kutumia ushahidi, takwimu katika kuwasilisha hoja za," amesema Sonda.




*Deogratius Mahinyila*

# Dkt Nchimbi azua...

Inatoka Uk. 9

"Kwangu mimi kila jibu linazua swali, mfano makamu (wa rais) amesema mheshimiwa rais anaitaka kwa sababu iliwekwa kwenye ilani, sasa kama rais anaitaka, kwa nini wananchi waipambanie?

"Swali la pili; tunapambana na nani ili kuipata? Swali la tatu; makamu kusema ni jambo zuri, lakini anaposema rais anaitaka, kwa nini rais mwenyewe hasemi moja kwa moja?" amehoji Askofu Bagonza.

Kiongozi huyo wa kiroho amesema kumekuwa na kigugumizi juu ya jambo hilo, hivyo ni wakati sasa Rais Samia mwenyewe aseme kuliko kuacha wasaidizi wake wamsemee.

**Bavicha wanena**

Mwenyekiti wa Baraza la Vijana wa Chadema (Bavicha), Deogratius Mahinyila amekuwa na masuala mbalimbali kumhoji Dkt. Nchimbi kutokana na kauli yake.

"Tuipiganie Katiba Mpya kivipi wakati (Tundu) Lissu (mwenyekiti wa Chadema) aliipigania akafunguliwa kesi ya uhaini? Tukomae na Katiba Mpya kivipi wakati vijana walipokomaa mwaka jana walipigwa risasi?

"Tupiganie Katiba Mpya gani ambayo vijana wa Mbeya, Mwanza, Iringa na mikoa mingine wakifanya hivyo wanafunguliwa kesi ya ugaidi na uhaini..?

"Tuipiganie Katiba Mpya wakati Dkt. Melkisedek Kaijage wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) amewaambia wanafunzi wake darasani kuwa kuandamana ni haki ya kikatiba, leo amefunguliwa kesi ya ugaidi," anahoji Mahinyila.

**UVCCM**

Katikati ya mjadala mkali hususani kwenye mitandao ya kijamii, ameibuka Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Mohamed Ali Kawaida, akikosoa kauli ya Dkt. Nchimbi na kumuonyesha kama mtu mbinafsi.

Katika andiko refu aliloliweka kwenye mitandao ya kijamii, Kawaida anasema chama cha siasa ni taasisi inayojengwa juu ya misingi ya utaratibu wa ndani na uwajibikaji wa pamoja.

Ingawa hakumtaja moja kwa moja Dkt. Nchimbi kwenye andiko lake, lakini maneno aliyoandika yanaakisi kauli iliyotolewa na makamu huyo wa rais.

"Uimara wa taasisi haupimwi kwa umaarufu wa mtu mmoja isipokuwa kwa uwezo wake wa kulinda taratibu, utamaduni na maamuzi ya pamoja..."

"Pale ambapo viongozi au makada huanza kutanguliza malengo binafsi kuliko maamuzi ya taasisi, hujitokeza kile kinachoitwa personalisation of power (kujitwika nguvu binafsi); hali ambayo maslahi ya mtu binafsi hupewa uzito kuliko uhalali wa taasisi,"amesema Kawaida.

Mchakato wa kuandika Katiba Mpya ulianza mwaka 2011 chini ya Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete lakini ulikwama mwaka 2014 kabla ya kupigiwa kura ya maoni.

Rais Samia amewahi kusema kuwa mchakato huo utafufuliwa ili kuhakikisha Katiba Mpya inapatikana kabla ya uchaguzi wa mwaka 2030.

**Wanaharakati**

Wanaharakati, wataalam na wachambuzi wa masuala ya Katiba na siasa, wameonyesha wasiwasi kuhusu hatma ya Tanzania kuwa na maridhiano ya kweli sambamba na Katiba Mpya.

Mwalimu wa Chuo cha Diplomasia Kurasini Dar es Salaam, Deus Kibamba, anasema ingawa anaunga mkono mazungumzo ya Dkt. Nchimbi, lakini akaibua hoja kadhaa, huku akihoji lini zoezi hilo la upatikanaji wa Katiba Mpya litaanza.

Inaendelea Uk. 15

# Dkt Nchimbi azua...

Inatoka Uk. 14

"Naona anajaribu kuzungumza kwamba Tume ya Jaji Othman Chande imesema Katiba mpya ipatikane 2028, na yeye (Makamu wa Rais) anasema pambaneni tuipate mwaka 2028 ili itumike kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu..."

"Mimi nasema kama Katiba Mpya inatakiwa iwe sehemu ya kuleta mwafaka wa Tanzania, ilitakiwa ipatikane jana asubuhi," anasema Kibamba ambaye pia ni mwanaharakati wa masuala ya Katiba na haki za binadamu wakati akizungumza na ITV.

Naye Wakili William Maduhu anasema kauli ya Makamu wa Rais Dkt. Nchimbi inatoa mwanga kwamba pengine anachokizungumza hata rais pia anakiunga mkono.

Maduhu anasema makamu wa rais ni Mtanzania na ni raia kama wananchi wengine, hivyo ana haki ya kuwa na maoni kama mwananchi mwingine yeyote.

"Lakini la pili ni kwamba ni kiongozi wa kitaifa, ni namba mbili katika nchi, kwa hiyo anapotoa hata kama ni maoni, inakuwa inaelekeza, inaashiria mwanga fulani huko mbele.

"Lakini swali la msingi ni kwamba mbali na makamu wa rais na hata rais mwenyewe kuonyesha kuwa ana dalili za utashi huo wa kisiasa, swali ni kwamba je, CCM na serikali yake iko tayari kwa hilo?" anauliza Wakili Maduhu.

Mchambuzi mwingine, Mwalimu Ntezimana Kiyogela, anasema Dkt. Nchimbi ametambua shida za wananchi kwa sababu maridhiano ambayo wananchi wanayataka siyo ya wanasiasa, bali ni kati ya wananchi pamoja na serikali yao.

"Kauli ya makamu wa rais imekuja wakati mwafaka kwa sababu amesemea kipengele cha Katiba Mpya na ni kweli Watanzania tunatakiwa kuipambana kwa sababu ni moja kati ya matakwa ya wananchi kwa muda mrefu," anasema Mwalimu Kiyogela.

## Mitego ya Senene...



*Mitego ya kukamatia senene ambayo hufungwa taa maalum nyakati za usiku ikiwa imefungwa eneo la Izigo mkoani Kagera ikisubiria msimu wa senene kuanza kati ya mwezi Septemba na Disemba kama ilivyokutwa juzi. Biashara ya senene inasaidia kuongeza vipato kwa vijana na wanawake.*

Habari

# Wachina kutumia Bandari ya Kigoma kubeba madini DRC




Na Mwandishi WETU

MELI mpya nne ambazo zilizinduliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan katika Ziwa Tanganyika, zinamilikiwa na wawekezaji kutoka China.

Pambazuko linaweza kueleza kuwa kampuni hiyo, Zijin Mining Group, imejenga meli hizo nne kwa ajili ya shughuli zake za uchimbaji wa madini ambazo inaziendesha mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Wachambuzi wa masuala ya kiuchumi wamelidokeza Pambazuko kuwa hatua hiyo siyo ya kushangaza katika kipindi hiki ambacho China inapambana kuongeza umiliki wake katika biashara ya madini, hasa madini adimu, ambayo yanapatikana kwa wingi katika maeneo mengi mashariki mwa DRC.

Katika kudhihirisha kuwa haina utani kwenye suala la biashara ya madini, kampuni hiyo tayari ilishaanza usafirishaji wa madini hata kabla meli hizo hazijazinduliwa rasmi.

Akizungumza katika uzinduzi wa meli hizo uliofanywa na Rais Samia wiki iliyopita, makamu wa rais wa kampuni hiyo, Qiu Guozhu, ameelezea hatua waliyopifikia kuwa ni muhimu katika safari yao ya kuendeleza shughuli za uchimbaji na usafirishaji wa madini katika eneo la Afrika Mashariki.

Inaelezwa kuwa meli hizo ni sehemu ya mpango wa usafirishaji wa kampuni hiyo unaoziweka pamoja njia mbalimbali za usafirishaji ikiwemo ardhini na majini.

Mradi huo ulitekelezwa baada ya kampuni hiyo ya Zijin Mining kuingia makubaliano na Serikali ya Tanzania na kukubaliwa kukodishwa na kuendesha shughuli katika sehemu ya Bandari ya Kigoma na kituo cha kupokea mizigo cha Malindi katika Bandari ya Dar es Salaam.

Chini ya makubaliano hayo, pamoja na mambo mengine, kampuni hiyo ilikubali kujenga meli zenye uwezo wa kubeba tani 2,000 za shehena na kuboresha Bandari ya Kigoma na pia kituo cha kupokelea mizigo cha Malindi.

Pia makubaliano hayo yalihusisha uendelezaji wa yadi za kuhifadhi mizigo, maghala na miundombinu mingine kwa kuiwekea vifaa vya kisasa vya kupakua na kupakia mizigo.

Pia kampuni hiyo ilitakiwa kuweka mfumo wa kisasa wa kudhibiti uendeshaji wa maeneo hayo ili kuongeza ufanisi wake.

**Kujengwa meli nne**

Kama sehemu ya utekelezaji wa makubaliano hayo, kampuni hiyo iliingia mkataba na kampuni nyingine ya China, Shandong Xinneng Shipbuilding, kujenga meli hizo nne kwa gharama ya dola za Marekani milioni 10.

Meli hizo zilijengwa nchini China na kisha vifaa vyake kusafirishwa na kuja kuunganishwa Ziwa Tanganyika.

Inaendelea Uk. 17

# Wachina kutumia...

Inatoka Uk. 16

Meli ya kwanza, iliyopewa jina la Jin Hang 1 (au Golden Voyage 1) iliingizwa majini Novemba 11 mwaka jana, na meli ya pili - Jin Hang 2 – yenyewe iliingizwa majini Disemba 23, 2025.

Meli nyingine mbili, Jin Hang 4 na Jin Hang 3 nazo zilikamilishwa na kuingizwa majini mnamo Machi 16 na 17, 2026 mtawalia.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa meli hizo wiki iliyopita, Makamu wa Rais wa Zijin Mining, Qiu Guozhu, alisema kampuni hiyo imejizatiti kufanya maboresho ya Bandari ya Kigoma na kituo cha Malindi kulingana na mkataba wa ukodishwaji waliosaini na serikali.

"Mradi huu utafungua njia ya usafiri wa kibiashara kuunganisha eneo la Asia ya Kati na Mashariki na Afrika. Madini yatasafirishwa kutoka Bandari ya Kalemie nchini DRC kuvuka Ziwa Tanganyika mpaka Bandari ya Kigoma na kisha hadi kituo cha Malindi, na baada ya hapo kuingia kwenye safari ya kimataifa kuelekea mabara mengine duniani," Qiu alifafanua.

Akaongeza; "Mfumo huu wa usafirishaji unaohusisha usafiri majini na ardhini utaimarisha pia mfumo wa lojistiki wa kanda na hivyo kusukuma uchumi kwa kasi kubwa kwa upande wa Tanzania na majirani zake."

Meli hizo ambazo kila moja ina urefu wa meta 70 na upana wa meta 15, zinaendeshwa na kampuni tanzu ya Zijin iitwayo Golden Voyage Logistics.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, amesema kampuni hiyo inatarajiwa kuleta meli nyingine mbili.

"Meli hizi zitakuwa na faida kubwa kwa sababu katika Ziwa Tanganyika kulikuwa na meli kubwa nne tu, tatu zina uwezo wa kubeba tani 2,000 na moja inabeba tani 3,000 za shehena..."

"Kwa hiyo, kuingia kwa meli hizi nne tutakuwa na meli kubwa nane ndani ya Ziwa Tanganyika na hiyo itasaidia kuongeza kiwango cha mizigo inayosafirishwa kati ya Kigoma na Kongo," alisema Mbossa wakati wa sherehe za uzinduzi wa meli hizo.

Mbossa akaongeza; "Kwa hiyo sisi ni sehemu ya mradi mkubwa wa kusafirisha shehena ya madini. Tuliwaomba wafanye kazi hiyo kwa sababu wanajenga pia bandari ya Kalemie na pia wanajenga bandari hii ya Kigoma…"

"Pia wanajenga barabara yenye urefu wa kilometa 500 kutoka Manono nchini DRC ambako ndiko kuna migodi yao ya madini hadi bandari ya Kalemie."

Taarifa ambazo zimelifikia Pambazuko zinaeleza kuwa tayari kampuni hiyo ya Zijin Mining imeshaanza kuzitumia meli hizo na Bandari ya Kigoma kusafirisha shehena ya madini kutoka katika machimbo yake huko mashariki mwa DRC.

Wapasha habari hao walidokeza kuwa meli hizo zilizinduliwa tayari zilikuwa zimeshasafirisha shehena ya madini aina ya Lithium kupitia Ziwa Tanganyika kupitia Bandari ya Kigoma.

Madini hayo yalitokea katika mradi wa Manono North East Lithium Project, uliopo katika eneo lenye moja ya eneo linaloongoza duniani kwa wingi wa hazina ya madini hayo ardhini.

Mradi wa Manono, ambao ni wa ubia kati ya Zijin Mining inayomiliki asilimia 54.9 ya hisa na Serikali ya DRC, unatajwa kuwa moja ya miradi utakaoneemesha korido hii ya usafiri kupitia Ziwa Tanganyika na Bandari ya Kigoma.

### Ushindani na Lobito

Kukamilika kwa korido hii ya usafiri kunaiweka Tanzania katika nafasi ya kushindana na korido nyingine ya usafiri ya Lobito ambayo inaiunganisha DRC na Bahari ya Atlantiki.

Korido ya Lobito inapigiwa upatu sana na wadau wa usafirishaji katika eneo hili la Afrika ikitajwa kuwa yenye ufanisi mkubwa kwani inaunganishwa kwa njia ya reli.

Lakini uzuri wa korido ya Kigoma ni ufupi wa safari yake kufika Bandari ya Dar es Salaam na hivyo kuwezesha shehena kufika mapema zaidi hasa kuelekea Asia na Mashariki ya Mbali.

Akizindua meli hizo, Rais Samia alibainisha kuwa Tanzania ipo kwenye eneo zuri kijiografia kufanikisha biashara katika ukanda huu wa Afrika.

"Kijiografia nchi yetu Tanzania ipo katika eneo na kuwezesha na kurahisisha biashara na nchi jirani na kwa asili, Mungu ametengeneza hivyo, lakini katika masuala ya sera na sheria, ni juu yetu kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara barani Afrika na tunaelekea huko," alisema.

# Mradi wa gesi kuzalisha dizeli, mafuta ya ndege kuanza



*Jack Pemba*

**Na Mwandishi WETU**

KUCHELEWA kuanza kwa mradi wa kusambaza gesi asilia kunachelewesha miradi mingine kadhaa mikubwa, Pambazuko limedokezwa.

Moja ya miradi mikubwa ambao utekelezaji wake unasubiri kukamilika kwa mradi wa kusambaza gesi asilia ni ule unaojengwa na kampuni kutoka Canada, unaohusisha ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza mafuta ya dizeli na mafuta ya ndege kutokana na gesi asilia.

Hatua za awali za uwekezaji wa mradi huo mkubwa wa kutumia gesi asilia kuzalisha mafuta hayo zimekamilika, lakini sasa umekwama ukisubiri uhakika wa upatikanaji wa gesi asilia.

Kampuni hiyo ya Canada, imeshakamilisha hatua kadhaa muhimu, lakini imeshindwa kuendelea na ujenzi wa kiwanda hicho ikisubiri uhakika wa upatikanaji wa gesi asilia ambayo ndio malighafi muhimu katika utekelezaji wa mradi huo.

Mradi huo wa kuzalisha dizeli na mafuta ya ndege unatekelezwa na kampuni ya Canada ya Rocky Mountain GTL, ikishirikiana na mshirika wake wa Afrika, Memnon Africa, pamoja na kampuni mwenza ya nchini, Rithi Tanzania Group Limited.

Taarifa ambazo Pambazuko imezipata zinabainisha kuwa wawekezaaji hao tayari wameshakamilisha utafiti wa awali (feasibility study) kwa kushirikiana na serikali kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda hicho cha kubadilisha gesi asilia kuwa mafuta kimiminika (GTL).

Kampuni hiyo hivi sasa inasubiri kuingia makubaliano ya kimkataba wa kusambaziwa gesi asilia na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Pambazuko limedokezwa kuwa kwa hatua ya uwekezaji ilipofikia, mkataba huo wa upatikanaji wa gesi asilia ni muhimu sana kwa wawekezaji ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa malighafi muhimu katika shughuli zao.

Mradi huo ambao una thamani ya dola za Marekani milioni 420, unatarajiwa kuwa mkombozi mkubwa katika sekta ya nishati nchini kwani kuna uwezekano Tanzania ikaacha kuhangaika kuhusu upatikanaji wa dizeli na mafuta ya ndege kwani bidhaa hizo zitazalishwa nchini.

Lakini wakati kampuni hiyo ikisubiri kuhakikishiwa upatikanaji wa gesi asilia, Mkurugenzi Mkuu wa TPDC, Mussa Makame, hivi karibuni alinukuliwa na gezeti la The Citizen akiitaka kampuni hiyo kuwa na subira.

Alisema TPDC hivi sasa ina miradi mingine ya kipaumbele ya kuharakisha uzalishaji wa umeme.

"Tutatia saini mkataba huo pale tu tutakapojiridhisha kuwa tuna gesi ya kutosha kuendesha mradi huo. Kwa sasa, tunashuhudia ongezeko kubwa la mahitaji ya umeme, na kipaumbele chetu ni kutumia gesi asilia kufua umeme," Makame aliliambia The Citizen.

**Inaendelea Uk. 19**

# Mradi wa gesi...

Inatoka Uk. 18

TPDC ni shirika la umma ambalo limepewa dhamana ya kusimamia rasilimali ya gesi asilia nchini.

Akizungumza na Pambazuko hivi karibuni, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Memnon Tanzania, Jackson Pemba, alisema teknolojia hiyo ya kubadilisha gesi kuwa mafuta ni muhimu sana kwa Tanzania na nchi nyingi za Afrika wakati huu dunia ikiwa katika shida ya upatikanaji wa mafuta kutokana na migogoro kama inayoshuhudiwa huko Iran, Ukraine na Russia.

Alisema baada ya kukamilika kwa utafiti huo, mashauriano yanaendelea kuhusu muundo na ujenzi wa kiwanda hicho mkoani Mtwara.

"Tayari tumeshahakikishiwa mtaji na taasisi tatu kubwa za kifedha ambazo ziko tayari kuunga mkono mradi wetu mara tu tutakapokuwa tayari kuendelea," alisema.

Teknolojia itakayotumika pia ina uwezo wa kuzalisha gesi ya 'hydrogen' ambayo ni muhimu katika uzalishaji wa mbolea, moja ya bidhaa ambazo tanzania inazihitaji kwa kiasi kikubwa.

Pemba alisema mradi unaopangwa kutekelezwa nchini ni sehemu ya mipango ya kampuni hiyo kujenga kiwanda cha kwanza cha mfano cha GTL barani Afrika.

Ameliamba Pambazuko kuwa kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mapipa 5,000 ya mafuta kwa siku, sawa na takriban lita milioni nane za dizeli kwa siku.

Kiasi hicho ni takribani sawa na kiasi cha mafuta ya dizeli ambayo yanatumika nchini kwa siku hivi sasa.


Tanzania ina akiba ya gesi asilia inayokadiriwa kufikia futi za ujazo trilioni 57.54, ambayo kwa kiasi kikubwa inatumika katika uzalishaji wa umeme na matumizi ya viwandani.

Kuanzishwa kwa kiwanda cha GTL kunaenda sambamba na mkakati wa taifa wa kuanzisha vyanzo mbadala vya nishati na kupunguza utegemezi wa mafuta kutoka nje.

Iwapo utakamilika, mradi huo wa kugeuza gesi kuwa mafuta utaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza barani Afrika kuwa na kutumia teknolojia hiyo.

Pemba ameliambia Pambazuko kuwa mradi huo unaweza kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya dizeli na mafuta ya ndege kwa nchi jirani.

"Tumejifunza nini kutokana na shida za mafuta ambazo Tanzania izimepitia tangu kupata uhuru? Tanzania ina gesi asilia ya kutosha inayoweza kubadilishwa kuwa dizeli na tayari kuna wawekezaji walioonyesha nia," alisema Pemba.



Habari

# Lissu ahenyesha mkuu wa gereza




Na Mwandishi WETU

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu amehenyesha Mkuu wa Gereza la Ukonga ambako yuko mahabusu.

Katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ambako kumehitimishwa siku tatu za kwanza za usikilizaji wa Shauri la Kikatiba Na. 7300 la mwaka 2026, Lissu amemhoji maswali kadhaa mkuu huyo wa gereza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza, Andrew Shabani Ntamamiro.

Shauri hilo lilifunguliwa na mawakili wa Tundu Lissu, wakipinga kile wanachodai kuwa ni ukiukwaji wa haki ya kufanya mashauriano ya siri kati ya wakili na mteja katika Gereza Kuu la Ukonga, Dar es Salaam.

Mawakili hao William Maduhu, Nashon Nkungu na Paul Kisabo wamefungus shauri dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamishna Jenerali wa Magereza, Mkuu wa Gereza la Ukonga.

Shauri hilo linatajwa kuwa moja ya mashauri muhimu ya kikatiba ambayo uamuzi wake unaweza kuweka mwelekeo mpya kuhusu mipaka ya mamlaka ya Jeshi la Magereza na haki za msingi za mahabusu wanaojiandaa kujitetea mahakamani.

Kesi hiyo inasikilizwa na jopo la majaji watatu linaloongozwa na Jaji Amir Mruma, akisaidiwa na Jaji Dk. Angelo Rumisha na Jaji Dk. Evaristo Longopa.

Siku ya kwanza: Wakili Maduhu aeleza vikwazo vya kumwona mteja

Usikilizaji ulianza Julai 20, 2026 kwa ushahidi wa Wakili William Maduhu, ambaye alieleza changamoto mbalimbali walizokumbana nazo katika jitihada za kumwona na kushauriana na mteja wao gerezani – Tundu Lissu.

Katika ushahidi wake, Maduhu alieleza kuwa mara kadhaa walinyimwa fursa ya kuonana na Lissu, hali aliyosema imeathiri maandalizi ya utetezi wake.

Katika dodoso, shahidi huyo aliulizwa na Lissu iwapo anadhani kuwa hali yake ya ulemavu wa ngozi inaweza kuwa moja ya mambo yaliyosababisha azuiwe kumuona mteja wake gerazani.

Swali hilo lilimfanya shahidi huyo kushindwa kujizuia na kububujikwa machozi, akisema mazingira hayo yalikuwa magumu zaidi kutokana na hali yake ya ualbino.

Alidai kuwa mashauriano kati ya wakili na mteja yanapaswa kufanyika kwa uhuru na faragha, bila kuingiliwa na mamlaka yoyote.

Siku ya pili: Mawakili waeleza jinsi mawasiliano yao yanavyodhibitiwa

Siku ya pili ya usikilizaji, Julai 21, ilitawaliwa na ushahidi wa mawakili Nashon Nkungu na Paul Kisabo.

Katika ushahidi wake, Kisabo alidai kuwa mikutano yao na Lissu imekuwa ikifanyika chini ya ulinzi mkali unaofanana na ule unaotumika kwa wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo.

Inaendelea Uk. 21

# Lissu ahenyesha...

Inatoka Uk. 20

Alieleza kuwa maafisa wa magereza wamekuwa wakihudhuria katika chumba cha mazungumzo, huku kukiwa na kamera za CCTV na matumizi ya simu za ukutani zilizotenganishwa na kioo.

Kwa mujibu wake, mazingira hayo yameondoa kabisa usiri unaopaswa kuwepo kati ya wakili na mteja.

Mbali na hilo, Kisabo alidai kuwa baadhi ya nyaraka muhimu za kisheria zimekuwa zikizuiliwa zisifikishwe kwa Lissu.

Alizitaja nyaraka hizo kuwa ni pamoja na Ripoti ya Tume ya Jaji Chande, maoni ya Kikosi Kazi cha Umoja wa Mataifa kuhusu Uzuiaji wa Kiholela (UN Working Group on Arbitrary Detention) yaliyodai kuwa kushikiliwa kwa Lissu ni kinyume cha sheria, pamoja na nyaraka mbalimbali za Jumuiya ya Madola zinazohusu haki zake.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali, Stanley Kalokola, Kisabo alisema walikuwa tayari wamewasilisha malalamiko yao kwa viongozi wa magereza lakini hakuna hatua zilizochukuliwa, jambo lililowalazimu kufungua shauri hilo Mahakama Kuu.

**Siku ya tatu:** Lissu amhoji mkuu wa gereza

Siku ya tatu, Julai 22, iligeuka kuwa moja ya siku zenye mvutano mkubwa baada ya Tundu Lissu mwenyewe kumhoji Mkuu wa Gereza la Ukonga, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza Andrew Shabani Ntamamiro.

Lissu alianza kwa kumhoji kuhusu msingi wa kisheria wa uendeshaji wa magereza, akirejea Sheria ya Magereza na Kanuni za Magereza za mwaka 1968.

Alimtaka shahidi huyo kueleza kama kuna kundi la wafungwa wanaoitwa Prisoners of Security Importance au wafungwa wenye uzito wa kiusalama.

Ntamamiro alikiri kuwa kanuni za magereza zinatambua makundi matatu pekee ya wafungwa, ambayo ni wafungwa vijana, wafungwa wa mfano na wafungwa wa kawaida.




*Mkuu wa Gereza la Ukonga, Andrew Ntamamiro (wa pili kushoto)*

Aidha, alikiri kuwa Mkuu wa Gereza wala Kamishna wa Magereza hawana mamlaka ya kubuni makundi mapya ya wafungwa nje ya yale yaliyowekwa kisheria.

**Hoja ya kusikilizwa mazungumzo**

Hoja iliyochukua muda mrefu zaidi ilikuwa madai kwamba maafisa wa magereza walikuwa wakisikiliza mazungumzo ya siri kati ya Lissu na mawakili wake, jambo ambalo lilikanushwa na Ntamamiro.

Inaendelea Uk. 22

■ Habari

# Lissu ahenyesha...

Inatoka Uk. 21

Katika hoja yake, Lissu alimuuliza Ntamamiro kama ana tatizo lolote la kusikia.

Ntamamiro alijibu kuwa hana tatizo lolote na ana uwezo mzuri wa kusikia.

Lissu aliendelea kuuliza kama Jeshi la Magereza linaweza kuajiri mtu asiyeona au asiyeweza kusikia.

Ntamamiro alijibu kuwa haliwezi kufanya hivyo isipokuwa pale mtu anapopata matatizo akiwa tayari kazini.

Kutokana na majibu hayo, Lissu alidai kuwa kwa kuwa maafisa wote waliokuwa ndani ya chumba wana uwezo wa kawaida wa kusikia, haiwezekani wasiwe wamesikia mazungumzo yake na mawakili.

Alikwenda mbali zaidi kwa kumsomea Ntamamiro sehemu ya kiapo chake mwenyewe kilichoonyesha kuwa maafisa hao walikuwepo ndani ya chumba, tofauti na ushahidi wake wa mdomo uliodai baadhi yao walitoka nje.

Alipotakiwa kutaja waliobaki ndani ya chumba, Ntamamiro alisema hakumbuki.



### Zuio la viongozi wa Chadema

Lissu pia alimhoji shahidi kuhusu sababu za kuwazuia viongozi wa Chadema akiwemo Makamu Mwenyekiti John Heche, Katibu Mkuu John Mnyika na Naibu Katibu Mkuu Amani Golugwa kumtembelea gerezani, pamoja na baadhi ya mawakili wake.

Ntamamiro alisema hawezi kuwaruhusu kuingia gerezani.

Kauli hiyo ilisababisha Jaji Amir Mruma kuingilia kati na kumuuliza kama ana amri yoyote ya mahakama inayomzuia kufanya hivyo.

Alipojibu kuwa hana amri hiyo lakini bado hawezi kuwaruhusu, Jaji Mruma alionyesha kutoridhishwa na msimamo huo.

“Unaiambia mahakama hii kwamba huwezi kuwaruhusu bila kuwa na amri ya mahakama? Una maana hiyo kweli?” alihoji Jaji Mruma.

Baada ya mahojiano hayo, Ntamamiro aliomba radhi kwa mahakama.

### Hoja kuu inayoamuliwa

Kiini cha shauri hili ni iwapo hatua zinazochukuliwa na Jeshi la Magereza kwa madai ya kulinda usalama zinaweza kuhalalisha kuingilia mawasiliano ya siri kati ya wakili na mteja.

Walalamikaji wanadai haki hiyo imekiukwa kwa kusikilizwa mazungumzo yao, kuwepo kwa maafisa wengi katika mikutano yao na kuzuiliwa kwa nyaraka muhimu za kisheria.

Kwa upande wake, Serikali imeendelea kusisitiza kuwa hatua zote zinazochukuliwa gerezani zinalenga kulinda usalama wa taasisi hiyo.

### Kesi yenye athari kwa mfumo wa haki

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Septemba mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na kupangiwa tarehe ya uamuzi.

Wachambuzi wa sheria wanaona kuwa uamuzi utakaotolewa katika shauri hili unaweza kuwa rejea muhimu katika mfumo wa haki jinai nchini, hususan kuhusu haki ya mahabusu kupata utetezi wa haki kupitia mawasiliano ya siri na mawakili wao.

# Bodi yadhibiti sukari yenye mchanga

**Na Mwandishi WETU**

MKURUGENZI wa Bodi ya Sukari, Prof. Kenneth Bengesi, amesema hatua zimeshachukuliwa kudhibiti sukari iliyobainika kuwa na mchanga.

Akizungumza na Pambazuko wiki iliyopita, Prof. Bengesi amesema bodi yake ilichukua hatua haraka baada ya kupokea malalamiko ya kuwepo kwa sukari yenye mchanga.

Profesa Bengesi aliliambia Pambazuko kuwa hajui tatizo limeanzia wapi, ingawa tayari tatizo hilo lilishashughulikiwa kwa wakati na sukari iliyobainika kuwa na kasoro iliondolewa sokoni hasa iliyokuwa kwenye hazina ya wauzaji wa jumla.

Amesema mamlaka zote zinazohusika na uingizaji na ukaguzi wa sukari ikiwemo Tume ya Atomiki ambayo hukagua mionzi, Mamlaka ya Viwango (TBS), Mamlaka ya Mapato (TRA) na Mamlaka ya Bandari (TPA) kila moja hufanya kazi yake ipasavyo, ingawa kuna uwezekano wa kuwepo hali ya udanganyifu ambapo ikibainika hatua kali huchukuliwa.

“Mimi kwa upande wangu, Bodi ya Sukari imetekeleza wajibu wake ipasavyo kwa kutoa vibali vinavyostahili na kuhakiki kiasi cha sukari kilichoingia nchini, majukumu mengine yanabaki kwa taasisi nyingine za kuhakiki ubora na usalama...”

“Katika hatua ya awali, ni kweli walipata taarifa kutoka kwa baadhi ya wananchi na walizipeleka TBS ambao kwa taarifa, walifanya ukaguzi na baada ya kubaini walidhibiti hadi kwa wauzaji wa jumla ambao tayari kwa wakati huo walishanunua mzigo na ulirejeshwa kwa wahusika. Hiyo ndiyo taarifa ninayoijua,” amesema.

Alieleza kuwa tatizo la sukari inayowezwa kuwa na viambata vya mchanga ilibainika kuwa inatoka Brazil na tatizo hilo halikuikumba Tanzania pekee, kwa kuwa kwa taarifa zilizopo sukari hiyo iliingizwa pia Kenya...”

“Kwa hiyo tatizo lilikuwepo. Ila inaonekana linakuzwa, kwa sababu tayari lilishadhibitiwa. Hata kampuni moja inayotajwa inaonekana kuwa kuna njama za kuchafuana kwa sababu siasa ya sukari ni ngumu...”

“Lakini nikufahamishe tu hii siyo mara ya kwanza, kwa miaka mingi tatizo limekuwa likijitokeza na limekuwa likidhibitiwa mapema...”

“Kwa hiyo wananchi waendelee kuwa na imani kwa sababu mamlaka ziko macho na zinafanya kazi muda wote,” alisisitiza.

Prof. Bengesi alitoa ufafanuzi huo kufuatia habari iliyoandikwa kwenye gazeti hili kwa wiki mbili ikieleza hofu iliyoibuka miongoni mwa wananchi, kwamba watumiaji wa sukari, kwa karibu miezi miwili sasa.

Malalamiko hayo ya sukari yenye mchanga yalifikishwa Pambazuko na gazeti hilo kuanza uchunguzi wake na kubaini kuwepo kwa sukari hiyo.

Uwepo wa sukari hiyo inayolalamikiwa kuwa na mchanga umeshuhudiwa na watumiaji wengi, ambapo kwa watumiaji wa chai wamekuwa wakilalamikia kuwepo kwa mabaki ya mchanga kwenye vikombe mara wanapoitumia.

Pia, watumiaji wa bidhaa za ngano, ambao wamekuwa akilalamikia mchanga katika mikate, keki, maandazi na bidhaa nyingine za ngano zinazotengenezwa kupitia sukari hiyo.

Katika uchunguzi wa Pambazuko kuhusu tatizo hilo, baadhi ya watengenezaji wa bidhaa hizo walieleza kuwa wamebaini tatizo hilo linatokana na matumizi ya sukari ambayo imekuwa si salama.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwango nchini (TBS), Dkt. Ashura Katunzi, aliliieleza Pambazuko kuwa ni kweli wamepata taarifa ya kuwepo kwa sukari hiyo yenye mchanga kwenye mzunguko wa bidhaa hiyo na tayari walishachukua hatua za awali za ufuatiliaji.



Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

# Kabla ya mteja, mfanyakazi anaipenda bidhaa?

NILIKUWA katika mkutano wa wakuu wa kampuni moja Msasani, Dar es Salaam, nikimsikiliza mkurugenzi akilalamika kwa uchungu kuhusu wafanyakazi wake.

"Watu hawa hawaielewi kampuni," alisema huku akigonga meza. "Tumeweka mabango makubwa barabarani na kulipia matangazo ya redio, lakini bidhaa zetu bado hazipendwi sokoni kama tunavyotaka."

Nikamuuliza; "Wafanyakazi wako wenyewe wanaipenda kampuni?"

Kimya kilitawala, mmoja wao alinitazama kana kwamba nimemuuliza kitendawili cha kale kisicho na jibu.

Ukweli ni kwamba biashara nyingi hazianguki kwanza sokoni; huanguka ofisini. Kama timu inavyojengwa kambini kabla haijaonekana uwanjani, kampuni hujengwa ndani kabla haijatangazwa nje.

Unapoiona Simba au Yanga ikicheza vizuri, usidhani ni bahati ya siku hiyo, haya ni matokeo ya mazoezi, nidhamu na mazungumzo ya chumba cha kubadilishia nguo ambayo shabiki hayaoni.

Kampuni ni vivyo hivyo, mteja anayekutana na mfanyakazi wako dukani, ofisini au kwa simu, anakutana na zao la mazingira ya ndani.

Ikiwa kuna mkanganyiko, nje mtaonekana mmechanganyikiwa. Huwezi kuficha kampuni isiyo na mfumo, kama ambavyo jezi nzuri haiwezi kuficha timu isiyo na mbinu.

Kocha mmoja mstaafu aliwahi kuniambia; "Wachezaji wanaweza kucheza vizuri kwa msimu mmoja hata kama hawaelewani na kocha, lakini hali hiyo haidumu."

Taasisi nazo ziko hivyo, unaweza kuuza kwa muda licha ya wafanyakazi kutoelewa mwelekeo wako. Baadaye uchovu hujitokeza, mauzo hushuka na wateja huanza kuhoji.

Tatizo la mabosi wengi ni kudhani taarifa moja inatosha, wanaandaa mkakati kwa miezi mitatu, kisha wanauzindua kwa barua pepe na mkutano wa saa moja.

Kesho yake wanatarajia kila mfanyakazi awe ameuelewa na kuutekeleza. Hiyo ni sawa na kumfundisha mchezaji mbinu mpya dakika tano kabla ya mechi, kisha kumlaumu anapokosea.

Mawasiliano ya ndani yanahitaji marudio, ufafanuzi na nafasi ya kuuliza, hayapaswi kuwa tangazo la jumla linalorushwa kama wimbo wa taifa.

Uongozi pia haupaswi kuwasikiliza wafanyakazi mara moja kwa mwaka kupitia dodoso refu, kisha kuyafungia majibu kabatini, mfanyakazi anahitaji kuona kuwa sauti yake inafika mezani na kuleta mabadiliko.

Nilipomuuliza mkurugenzi kama hupima ujumbe wake wa ndani umefika, umeeleweka na kuaminika, alishangaa. Mabosi wengi hupima mauzo, faida na gharama, lakini husahau kupima uelewa wa wafanyakazi.

Mawasiliano yasiyopimwa ni kama mazoezi bila saa; unaweza kukimbia, lakini usijue kama unaboreka au unadumaa.

Kampuni hupoteza wateja siyo kwa sababu bidhaa ni mbovu, bali wakati mwingine mfanyakazi aliyepokea simu hana taarifa sahihi wala moyo wa kuisemea kampuni.

Mamilioni yaliyotumika kwenye matangazo yanaweza kuharibiwa na mazungumzo ya dakika tano.

Ieleweke kuwa chapa haiishi kwenye bango; huishi katika sauti ya mfanyakazi wa mwisho kwenye mnyororo.

Mfanyakazi anayesikilizwa hujenga; anayeamriwa tu huvumilia; wa kwanza huitetea kampuni hata nje ya kazi na wa pili husubiri muda wa kuondoka.

Kwa hiyo, kuwekeza katika mawasiliano ya ndani siyo anasa, huenda gharama yake isionekane mara moja kwenye hesabu, lakini matokeo yake huamua kama biashara itasimama imara au itaanguka.

Mwisho nikamwambia mkurugenzi; "Kabla hujauliza kwa nini wateja hawakupendi, jiulize kama wafanyakazi wako wanakupenda." Akanyamaza tena.

Huenda hilo ndilo jibu alilokuwa akilitafuta tangu asubuhi.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@ lothmakuza.co.tz***

Na Emmanuel JACOB



# Wenye ulemavu wana haki sawa na wengine



KWA muda mrefu, jamii imekuwa ikichukulia usaidizi kwa watu wenye ulemavu kama kitendo cha hisani au huruma.

Hata hivyo, mtazamo huu wa kiasili (Charity Model) unawashusha thamani na kuwafanya watazamwe kama "vitu vya kuhurumiwa" badala ya wanajamii wenye haki kamili sawa na wenzao waliojaaliwa viungo vyote.

Ili kuleta maendeleo ya kweli, ni lazima tubadilike na kuelekea kwenye mtindo unaozingatia haki za kibinadamu (Rights-Based Model), ambapo lengo kuu ni kuwekeza katika elimu jumuishi, mafunzo ya amali, na fursa za ajira.

Je, sekta ya tiba ya viungo na uwezeshaji wa watu wenye ulemavu inatazamwaje katika ukanda wetu?

Katika mazungumzo yangu na Emmanuel Mayakah, Mtaalamu wa Tiba ya Viungo aliyetembelea nchi zote za Afrika Mashariki, anaeleza kwa nini ni wakati wa kubadili mtazamo wetu kutoka kwenye huruma hadi kwenye haki.

Kutoa misaada bila masharti au bila kuhusisha juhudi za mtu mwenyewe huchukua utu wa mtu na kuunda uhusiano usio na usawa wa kutilia shaka uwezo wao.

Pindi watu wenye ulemavu wanapopewa nafasi ya kuwekeza katika safari zao za maisha kwa kiwango na uwezo wowote walionao inawapa hisia ya kumiliki hatima yao na kujenga kujiamini.

Mtindo wa zamani unachukulia kwamba mtu mwenye ulemavu hawezi kujitegemea. Mtindo wa kisasa wa kijamii (Social Model) unaweka wazi kuwa tatizo si ulemavu wa mtu, bali ni vikwazo vya kijamii na miundombinu vinavyomzuia kushiriki.

Badala ya kutoa misaada inayowafanya wawe wapokeaji tu, jamii inapaswa kuondoa vikwazo hivyo ili kila mtu ashiriki kikamilifu.

Misaada ya haraka hutoa nafuu ya muda mfupi tu bila kutatua tatizo la msingi la kutengwa kiuchumi. Mipango inayolenga kujenga ujuzi, kutoa suluhu za kifedha zilizoboreshwa, na kuimarisha uwezo wa kiuchumi ndiyo inayojenga kujitegemea kwa muda mrefu na endelevu.

Suala la ulemavu si la ukarimu wa jamii; ni suala la haki za kibinadamu. Kazi ya utetezi lazima ilenge kuwapa watu wenye ulemavu zana, fursa na mazingira yanayostahili ili washinde changamoto na kuishi kama wanajamii sawa na wengine.

Mwisho, ni wakati sasa kwa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na jamii kwa ujumla kubadili mtazamo wa kutoa msaada ya huruma ambayo wakati mwingine haishughuliki na kiini cha tatizo na kuwekeza kwenye mifumo jumuishi.

Watu wenye ulemavu hawahitaji huruma bali haki, fursa na mazingira wezeshi ili kuonyesha mchango wao katika ujenzi wa taifa na kujiamulia hatma ya maisha yao.

***Mwandishi: Emmanuel Jacob, Ofisa Mfiziotherapia (Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Tanzania Physiotherapy Initiative). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob.***

Bustani ya Sheria





Na Wakili Karim Gabriel Mussa

# Sakata la Wakili Fatma Karume – 1

"JE, wakili ana mipaka gani ya kutumia lugha kali mahakamani? Je, uhuru wa wakili kumtetea mteja wake una mwisho wake? Na ni wakati gani hoja za kisheria zinaweza kubadilika na kuwa kosa la kitaaluma?"

Maswali hayo ndiyo yaliibua moja ya migogoro mikubwa kuwahi kutokea katika taaluma ya uwakili nchini Tanzania.

Mgogoro huu uliomhusisha Wakili Fatma Karume, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahakama Kuu, Kamati ya Maadili ya Mawakili na baadaye Mahakama ya Rufani.

Hadi leo, kesi hizi zimeendelea kufundishwa Shule Kuu ya Sheria (Law School) kwa sababu zimeweka misingi muhimu kuhusu maadili ya wakili, mamlaka ya mahakama na haki za wakili anayeshitakiwa kwa utovu wa nidhamu.

### Mwanzo wa Mgogoro

Mwaka 2018, mwanaharakati Ado Shaibu (sasa mbunge), kupitia wakili wake, Fatma Karume, alifungua shauri Mahakama Kuu dhidi ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Adelardus Kilangi

Ado Shaibu alidai kuwa uteuzi wa Adelardus Kilangi kuwa mwanasheria mkuu ulikuwa umefanywa kinyume cha Katiba kwa sababu, kwa mtazamo wake, Kilangi hakutimiza sifa zinazotakiwa kushika nafasi hiyo.

Serikali haikujibu moja kwa moja hoja hizo. Badala yake iliweka mapingamizi ya awali ikidai kuwa Rais hawezi kushtakiwa kwa namna shauri lilivyofunguliwa; walioshtakiwa hawakuwa wahusika sahihi; hakukuwa na sababu ya msingi ya kufungua kesi na kwamba nafuu zilizoombwa haziwezi kutolewa na Mahakama.

Lakini wakati hoja hizo zikijadiliwa, jambo jingine likatokea ambalo baadaye lilibadilisha kabisa historia ya Fatma Karume.

### Maneno yaliyotikisa Mahakama

Katika hoja zake za maandishi, Fatma Karume alimwelezea Mwanasheria Mkuu kuwa ni "...far too junior...(bado hajakomaa kitaaluma)" na akaendelea kusema kuwa hana uzoefu wa kutosha kushika nafasi ya mwanasheria mkuu na kwamba ameshindwa kuishauri serikali ipasavyo.

Fatma hakuishia hapo, akaendelea; "ikiwa kesi hii itashindwa leo, tutairudisha baada ya rais kutoka madarakani. Huo ndio uzuri wa muda."

Serikali iliona maneno hayo siyo hoja za kisheria, bali yalikuwa mashambulizi binafsi dhidi ya mwanasheria mkuu.

**Swali likawa;** Je, wakili alikuwa akitetea maslahi ya mteja wake, au alikuwa amevuka mipaka ya maadili ya taaluma?

Mahakama Ilisema baada ya kusikiliza mapingamizi ya serikali, Mahakama Kuu ilikubaliana na upande wa serikali na kutupilia mbali kesi ya Ado Shaibu.

Lakini kabla ya kufunga jalada hilo, Jaji aligeukia suala la lugha iliyotumiwa na Fatma Karume.

Mahakama ilisema madai ya utovu wa nidhamu dhidi yake yalikuwa mazito kiasi kwamba yalihitaji kuchunguzwa rasmi na chombo chenye mamlaka ya kusimamia maadili ya mawakili.

Kwa kutumia mamlaka yake chini ya kifungu cha 22(2)(b) cha Sheria ya Mawakili, Jaji akatoa amri mbili muhimu; kwamba Fatma Karume asimamishwe kwa muda kufanya kazi ya uwakili na kutamka kwamba Msajili wa Mahakama apeleke suala hilo kwenye Kamati ya Maadili ya Mawakili ili lisikilizwe na kuamuliwa.

Uamuzi huo uliibua mjadala mkubwa nchini; Kwa mara ya kwanza, mmoja wa mawakili maarufu nchini alikuwa amesimamishwa kufanya kazi kwa sababu ya lugha aliyotumia katika maandishi ya mahakama.

Lakini huo haukuwa mwisho, ndiyo ulikuwa mwanzo wa mlolongo wa kesi saba tofauti, zilizofika hadi Mahakama ya Rufani na kubadilisha kabisa namna sheria za maadili ya mawakili zinavyofundishwa nchini Tanzania.

**Itaendelea...**

***Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com***



Na Rashid MTAGALUKA



# Kuna nini nyuma ya kauli ya Dkt Nchimbi?

KAULI ya Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi - ya kuwataka Watanzania "kupambana kupata Katiba mpya" imezua mjadala mpya katika medani ya siasa.

Siyo kwa sababu hoja ya Katiba mpya ni mpya, bali kwa sababu sasa inatamkwa na mmoja wa viongozi wakuu wa dola, wakati kwa miaka mingi imekuwa ikisukumwa zaidi na vyama vya upinzani, wanaharakati na asasi za kiraia.

Kauli hiyo inazua swali muhimu; Je, CCM imeanza kubadili msimamo wake kuhusu katiba mpya – kwa uwazi? Au ni kauli ya kisiasa inayolenga kutuliza mjadala unaozidi kushika kasi?

Kwa zaidi ya muongo mmoja, hoja ya katiba mpya imekuwa ikitajwa kuwa msingi wa kujenga mfumo wenye uwajibikaji, usawa wa kisiasa na taasisi imara za dola.

Lakini pamoja na ahadi na mijadala mbalimbali, mchakato huo haujawahi kukamilika. Ndiyo maana kauli ya Dkt. Nchimbi haiwezi kupimwa kwa uzito wa maneno yake pekee, bali kwa hatua zitakazofuata.

Katika mazingira ya sasa, ambapo upinzani unaendelea kuifanya katiba mpya kuwa ajenda yake kuu ya kisiasa, kauli ya Makamu wa Rais wa Tanzania inaweza kubadili mwelekeo wa mjadala. Endapo CCM itaamua kuibeba hoja hiyo kwa vitendo, upinzani utalazimika kutafuta hoja mbadala za kujiimarisha kisiasa.

Lakini kama kauli hiyo itaishia kuwa sehemu ya hotuba bila mpango wa wazi wa kuendeleza mchakato wa katiba mpya, basi itatazamwa kama mbinu nyingine ya kisiasa ya kupunguza presha ya umma.

Hata hivyo, Watanzania hawahitaji tena kusikia kuwa katiba mpya ni muhimu; hilo limezungumzwa kwa miaka mingi. Wanachohitaji ni ratiba, dhamira na hatua zinazoonekana. Historia ya kisiasa ya Tanzania imejaa kauli nzuri ambazo hazikufuatiwa na utekelezaji.

Kwa hiyo, kauli ya Dkt. Nchimbi inapaswa kuwa mwanzo wa mjadala mpya unaojikita kwenye vitendo badala ya maneno. Taifa halitapima uhalisia wa kauli hiyo kwa makofi ya hadhara, bali kwa uamuzi wa kufufua mchakato wa katiba mpya kwa uwazi, ushirikishwaji na maridhiano ya kitaifa.

Mwisho wa yote, swali si kama Watanzania wanahitaji katiba mpya, bali swali ni nani yuko tayari kuigeuza ahadi hiyo kuwa uhalisia? Historia itawakumbuka waliozungumza, lakini itawaheshimu zaidi waliochukua hatua.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***

Habari

# Tibaigana: Polisi watumie zaidi teknolojia za kisasa



Alfred Tibaigana

Na Mwandishi WETU

KAMANDA mstaafu wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Alfred Tibaigana, ameshauri kuimarishwa zaidi mafunzo ya kitaalam kwa askari ili kwenda na kasi ya teknolojia ya kisasa duniani.

Pia anashauri kipaumbele zaidi kiwekwe kwenye Sera ya Polisi Jamii, akisema itasaidia kuimarisha uhusiano wa askari na wananchi kuanzia ngazi ya chini, na ndiyo njia pekee ya kupunguza vitendo vya uhalifu katika maeneo mbalimbali nchini.

Katika mazungumzo maalum na Gazeti la Pambazuko nyumbani kwake Kijiji cha Buganguzi wilayani Muleba, Kagera hivi karibuni, Kamanda Tibaigana aliainisha masuala mbalimbali huku akisisitiza zaidi matumizi ya weledi, sheria, kanuni na miongozo katika utendaji wa jeshi hilo akisema kutaondoa migongano na taasisi zingine wakiwamo wanasiasa.

Kuhusu umuhimu wa polisi kuchangamana na raia, Kamanda Tibaigana anasema huo ni mfumo wa polisi kujenga urafiki na raia kupitia 'polisi jamii ngazi ya kata' na lengo ni kumfanya askari azoeane na raia, ajue shida zao na kama kuna matatizo ayapeleke kwa wakubwa wake ili yafanyiwe kazi.

Kamanda huyo mstaafu ambaye ni mmoja wa waanzilishi wa mfumo huo ambaye alipata mafunzo hayo nchini Marekani, anasema polisi kata hahusiki na kukamata wauza bangi, gongo…bali ni mtu kama maofisa wengine wa afya.."

"Kazi yake ni kujua matatizo kwenye eneo lake na kuyapeleka panapohusika ili yafanyiwe kazi. Hata hivyo, nadhani utekelezaji ndiyo changamoto kwa sababu unakuta askari kata anachukua ofisi, anakamata watu...:

"Kwenye mwongozo huyu anatakiwa kuwa rafiki, aende baa, ashiriki sherehe, harusi, misiba nakadhalika..."

"Nadhani huu utaratibu ukiimarishwa na kusimamiwa vizuri utazaa matunda. Kwanza unamfanya huyu askari achangamane na raia, wanamuona mwenzao, anashiriki shughuli za kijamii," anasema Kamanda Tibaigana.

Kuhusu teknolojia, anasema wakati akiwa kazini, uhalifu mkubwa waliokuwa wakipambana nao ulikuwa ni ujambazi wa kutumia silaha, lakini anaona vitendo hivyo kwa sasa vimepungua, na badala yake kuna ongezeko la uhalifu kwa njia ya mtandao, ambapo wahalifu wanaibia benki kwa kutumia teknojia ya simu na kompyuta wakiwa majumbani mwao.

Alipoulizwa maeneo ambayo Jeshi la Polisi linapaswa kufanyia kazi zaidi alisema kusimamia taratibu zinazoongoza utaratibu wa jeshi hilo ndiyo kitu kinachopaswa kupewa kipaumbele.

"Wanaweza ku-modify (kurekebisha) baadhi ya mambo kutokana na tunavyokwenda. Unajua dunia inakwenda kasi sana tofauti na enzi zetu, lakini pia behavior (tabia) za watu ni tofauti, hata crime (uhalifu) ni tofauti..."

"Miaka yetu yale tuliyokuwa tunapambana nayo, kwa mfano majambazi ya kutumia silaha, siku hizi siyasikii sana. Siku hizi watu wanatumia kompyuta kuchota fedha benki..."

Inaendelea Uk. 29

# Tibaigana: Polisi

Inatoka Uk. 28

"Kwa hiyo nadhani ni kuimarisha mafunzo, wawe na utaalam, wafanye kazi kwa mujibu wa taaluma zao, wasiingiliwe. Waachwe kwa sababu polisi ina miongozo yake mingi, sheria zipo. Sasa kama sheria na miongozo vipo nadhani waviimarishe hivyo," anasema Kamanda Tibaigana.

Kuhusu mambo ambayo Jeshi la Polisi linafanya vizuri zaidi, Kamanda Tibaigana alibainisha kuwa ingawa nyakati zimebadilika, lakini jeshi hilo linafanya mambo mengi mazuri.

"Inawezekana hata enzi zetu yalikuwa yanafanyika, lakini hayakujulikana, sasa yanajulikana zaidi. Kwa hiyo nadhani ni juu ya jeshi lenyewe kubadilika kwenda na wakati..."

"Wajitahidi kuwa imara kwa misingi ya miongozo ya jeshi la polisi. Vile vile wawe imara wakati mwingine wawashauri viongozi wa kisiasa, kwamba hiki tukienda hivi kitaleta madhara, kwa sababu wao ndiyo wana taaluma katika eneo husika.

### Jeshi na vyama vya siasa

**Swali:** Kamanda Tibaigana unazungumziaje tuhuma kuwa Jeshi la Polisi linahusishwa kukipendelea zaidi chama tawala?

**Jibu:** Jeshi linapaswa kusimamia kanuni, sheria na taratibu za utendaji wa Jeshi la Polisi kwa sababu kanuni zipo, sheria zipo. Na mojawapo ya sheria au kanuni inayoongoza Jeshi.

Ile ya kutii amri halali zinazotolewa na viongozi, kwa hiyo wakisimamia hapo haki itasikika kwa sababu hakuna kiongozi wa siasa atakayeamuru kitu ambacho si halali wakatekeleza.

Akiuzungumzia utaratibu wa askari kuishi mitaani na raia, kamanda Tibaigana alisema siyo jambo zuri kwani duniani kote askari wanapaswa wakae kambini, ingawa baadhi wanaweza kukaa uraiani kwa sababu maalum kama vile askari kanzu, wastaafu na polisi jamii.

"Utekelezaji wa hili ndiyo unaleta shida, lakini askari wengine wanakaa uraiani siyo kwa sababu ya kazi maalum au makachero ni kwa sababu makambi hayatoshi. Kazi ya kujenga kambi siyo kazi ya polisi ni kazi ya serikali..."

"Kwa sababu kwenye mkataba wa ajira, askari



anaambiwa atapewa makazi ya kuishi bure, sasa kama makazi hayapo, wanakwenda kupanga uraiani, maisha yao yanakuwa hatarini na baadhi yao wanaweza kuiga tabia zisizo sahii huko uraiani..."

"Kuhusu baadhi ya askari kuhusishwa na taasisi za kimataifa kukiuka haki za binadamu, alishauri maofisa wa polisi wafanye kazi zao kwa taratibu za sheria, kanuni.

"Kama ni matumizi ya nguvu kuna sheria inaruhusu, ni mazingira gani kwa sababu sheria inaruhusu polisi kuwa na silaha, na ataitumia wakati gani kwa ajili ya kujilinda yeye na kulinda raia..."

"Kama kuna mahali anaitumia kisheria, mimi sina shida, lakini ujue askari pia ni binadamu, ni kama watoto, mwingine anaweza akalipuka mwenyewe kwa sababu ana silaha akapiga mtu risasi ambako hakustahili. Lakini sheria na kanuni zipo atawajibishwa..."

"Hatuwezi kusema tuwanyang'anye silaha kwa sababu kuna mwingine anaitumia vibaya," ameongeza.

### Kugombea ubunge

Mwaka 2010 baada ya kustaafu Kamanda Tibaigana alijitosa kugombea ubunge. Alipotakiwa kueleza iwapo bado ana nia ya kufanya hivyo, alisema mpango huo ameshaufuta.

"Siasa ina muda wake, nadhani muda huo kwangu ulikwishapita, kwa sasa najikita zaidi kwenye shughuli zangu za kilimo na ufugaji.

## Barua za Wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Watendaji wasimkwamishe Dkt Mwigulu Nchemba

**Mhariri,**

NI rai yangu unipe nafasi japo pembeni ili niwabwekee na kuwakoromea baadhi ya watendaji na wasaidizi wanaotia dosari na kukwamisha kazi nzuri ya kukomesha kero inayofanywa na Waziri Mkuu, Mwigulu Lameck Nchemba.

Mei 25, 2026 Mwigulu alilitangazia taifa na dunia kiama kwa waporaji ardhi, akiwataka wale wote waliokanyaga haki na walionyang'anya ardhi kwa mabavu warejeshe na kuchukuliwa hatua.

Bila aibu, baadhi ya watendaji na wasaidizi hao, wamekuwa wakila njama wakibadili maagizo ya Dkt. Mwigulu ambaye ni mtendaji mkuu wa shughuli za serikali, na wakipotosha kwamba wasirejeshewe haki yao isipokuwa wapewe ardhi mbadala ili kuwalinda wahalifu na kuwasumbua wenye haki. Hatua ya watendaji hao ni ya kumdhalilisha Waziri Mkuu na kuichafua ofisi hiyo kubwa kwa wananchi na kutaka kumfanya asiaminike!

Hivyo tunamtazamisha waziri mkuu apembue watendaji na wasaidizi hao ambao wanajinufaisha kupitia mgongo wake.

Hayo yamejiri Kinyambwa Extension Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

**Ni mimi mkazi wa Kisasa, Dodoma**

## 'Media' zinazotangaza maudhui ya ngono zifungiwe

**Mhariri,**

SANAA kazi yake ni kuelimisha na kuburudisha jamii husika kwa kutoa mafunzo, jumbe na kukosa pale inapobidi lakini kwa sanaa ya Tanzania imekuwa kinyume chake.

Nasikitika msanii siyo kioo cha jamii tena na wala kazi ya sanaa siyo kuelimisha tena, bali imekuwa kuburudisha tu, inachosha kila ukiwasha redio au televisheni unakutana na nyimbo zilizojaa maudhui ya ngono tu mwanzo mwisho.

Kuna wakati unapata wasiwasi tunajenga jamii ya namna gani Basata mko wapi, kwanini mnafungia nyimbo za kukosa serikali tu na hizi za ujumbe wa ngono pia zisifungiwe kwa sababu wanatukana hadharani kwa kisingizio cha tafsida, hapana mnatuharibia jamii kwenye hili hapana.

**Scolastica Martin,**
**Kasulu, Kigoma.**

## Magari ya vyombo vya usalama viko juu ya sheria?

**Mhariri,**

INASIKITISHA kuona baadhi ya magari ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi na Magereza yamekuwa yakivunja sheria za usalama barabarani wazi wazi.

Inashangaza sana kwa sababu vyombo hivyo vya usalama ndiyo vinapaswa kuwa mfano wa usimamizi wa sheria.

Mfano mara kadhaa tumekuwa tukishuhudia magari ya vyombo hivyo vya usalama, yakipita kwenye barabara isiyo sahihi na hata kukiwa na taa nyekundu yamekuwa yakipita spidi kubwa na kumdharau hata askari anayeongoza magari.

Tunajiuliza wakati wote wao ndiyo wana haraka kuliko wananchi au wako juu ya sheria? Kibaya zaidi wakati mwingine magari haya yamekuwa yakisababisha ajali na hata pale wanapogonga gari yako wanaondoka bila kujali.

Tunaomba mamlaka husika ichukue hatua katika hili maana ni aibu kuona vyombo vya ulinzi na usalama, vinakuwa mstari wa mbele kuvunja sheria.

**Raphael Edison,**
**Mwenge, Dar es Salaam**


MOVE FOR DISABILITY
INCLUSION BY DESIGN 26'
WALK
with Us
29th August 2026
SPONSERED BY circleg
Kua mshiriki kwa Tshs 40,000/- Tu!
Nunua ticket yako kutumia Lipa Namba
MOVE FOR DISABILITY
6 1 2 4 6 6 1 0
INCLUSION BY DESIGN 26'
SPONSERED BY
circleg
Pambazuko

## Wazo Binafsi

# Nchimbi, kauli tamu yenye maswali mazito



Dkt. Emmanuel Nchimbi

Na Edward KINABO

NIMEPOKEA kwa mshangao na tahadhari kubwa kauli ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Emmanuel Nchimbi, iliyowataka wananchi na wanaharakati wa haki za binadamu "wapambane tupate Katiba mpya."

Kwa mtazamo wa haraka, kauli hiyo inaweza kuonekana ya kutia moyo kwa kuwa inakiri umuhimu wa Katiba mpya, lakini kwa tafakuri ya kina, ni kauli inayozua maswali makubwa kuhusu dhamira ya serikali katika kutekeleza ajenda hiyo.

Ni kauli inayomuacha Mtanzania ajiulize; je, kuna serikali nyingine yenye mamlaka ya kuzuia Katiba mpya ambayo hata makamu wa rais hawezi kuishawishi? Au serikali aliyomo ndiyo hiyo hiyo yenye mamlaka hayo lakini haina utashi wa kisiasa?

Kwa maoni yangu, kauli hiyo ina hitilafu kuu tatu.

Kwanza, inahamisha wajibu wa serikali kwenda kwa wananchi. Katiba mpya haitapatikana kwa wananchi kupambana vya kutosha, bali kwa serikali kutekeleza wajibu wake wa kuanzisha mchakato shirikishi wa kikatiba.

Jukumu la wananchi ni kushiriki kwa kutoa maoni na kuamua kupitia kura ya maoni, siyo kuishinikiza serikali itimize wajibu wake.

Pili, inaonesha upungufu wa utashi wa kisiasa. Serikali inayojali haiwasubiri wananchi wapambane ndipo iwape haki, usalama na ushiriki. Haki za msingi zinapaswa kulindwa kila siku, si kusubiri Katiba mpya.

Tatu, kauli hiyo inaifanya Katiba mpya kuwa ajenda ya kisiasa badala ya wajibu wa serikali. Siyo kawaida kwa kiongozi mwandamizi wa serikali kuwashauri wananchi wapambane ili kupata jambo ambalo serikali yake ina uwezo wa kulitekeleza leo ikiwa tu itafanya uamuzi wa kisiasa.

Katiba mpya siyo ajenda ya wanaharakati pekee, wala ya vyama vya siasa pekee. Ni ajenda ya taifa. Ni msingi wa kujenga utawala wa sheria, uchaguzi huru na wa haki, uwajibikaji wa viongozi na maendeleo yanayomgusa kila Mtanzania.

Badala ya kuwahamasisha wananchi waendelee kupambana, Watanzania wanatarajia kusikia serikali ikitangaza kwa uwazi mwanzo wa mchakato wa Katiba mpya, ratiba yake na dhamira yake ya kuufanikisha.

Katiba mpya siyo zawadi kutoka kwa watawala, bali haki ya Watanzania na kwamba haki hiyo haipaswi kuahirishwa.

Katiba Mpya ni Sasa.

***Mwandishi ni Katibu wa Sekretariati na Mkurugenzi wa Itikadi, Mafunzo na Elimu kwa Umma – Chaumma.***

# Waandishi wahimizwa kujiunga NSSF

Na Mwandishi WETU

RAIS wa Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi nchini (TUCTA), Tumaini Nyamhokya, amewataka wafanyakazi wa vyombo vya habari nchini kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) – Skimu ya Hiari, ili kuwalinda dhidi ya dhoruba za kiuchumi.

Nyamhokya amesema hayo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa semina maalumu ya kuhamasisha wafanyakazi wa sekta ya habari kujiunga na mfuko huo kwa kushirikiana Chama cha Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari (Jowuta).

Nyamhokya amesema takwimu zisizo rasmi zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wafanyakazi wa vyombo vya habari nchini hawako kwenye mfumo rasmi wa hifadhi ya jamii.

Alisema kwa wafanyakazi hao siku nguvu zinapoisha au kukumbwa na janga la ghafla kama vile kuugua au kupoteza uwezo wa kufanya kazi, maisha yao hugeuka kuwa "mlima mgumu kuupanda."

"Mpango huu wa Hifadhi ya Jamii wa Hiari (Hifadhi

Scheme) unaotekelezwea na NSSF ni mkombozi wa kweli, katika kujenga kesho yetu iliyo bora..."

"Waswahili wana msemo mmoja unaoeleza kuwa akiba haiozi, na akiba haimtupi mtu, hivyo basi, ili kuijenga kesho yako iliyo bora anza kuchimba msingi leo kupitia Hiyari Scheme kwani ni uwekezaji usiokuwa na hasara," anasema Nyamhokya kupitia kwa Mweka Hazina wa Tucta, Dkt. James Kalanje, aliyemwakilisha.

Ameongeza kuwa sekta ya habari ni mhimili mkuu wa demokrasia, uwazi, uwajibikaji na maendeleo ya nchi na kwamba wana habari ni kioo cha jamii, makocha wa fikra za wananchi, na sauti ya wanyonge.

Amebainisha kuwa wana habari wanafanya kazi usiku na mchana, kwenye jua na mvua, bila kujali hatari zinazowakabili, ili kuhakikisha taifa linapata taarifa sahihi kwa wakati.

Naye Kaimu Meneja wa NSSF Mkoa wa Kinondoni, Gerald Mkonyi, amesema NSSF ina mafao saba ambayo yamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni pensheni inayojumuisha pensheni ya uzee, pensheni ya ulemavu na pensheni ya urithi.

Pia kuna mafao ya muda mfupi ambayo ni mafao ya matibabu, msaada wa mazishi na mafao ya kupoteza ajira.

Akizungumzia kuhusu fao la matibabu amesema ili mwanachama ajiunge nalo anatakiwa kuchangia shilingi 30,000 kila mwezi na ikiwa atahitaji wategemezi wake (watoto wanne) wajiunge atachanga Shilingi 52,400 ambayo atalipia kila mwezi lakini pesa hiyo itamwezesha kufaidika na pensheni ya uzeeni.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Jowuta, Suleiman Msuya, amesema wanahabari ni kundi muhimu katika jamii kutokana na majukumu yake.

"Waandishi wa habari ni kundi muhimu na tunafanya kazi kubwa na nzuri kwa jamii lakini hatuijui kesho yetu usipoweka akiba unapostaafu hujui utakwenda kufanya nini hivyo mfuko huu ni muhimu kwetu," amesema Msuya.

Ameishukuru NSSF kwa kukubali kutoa elimu hiyo na kuwaomba kuwafikia wanachama wote wa Jowuta walioko pia nje ya Dar



*Wafanyabiashara wa ndizi wakipakia mikungu kuelekea sokoni kutafuta wateja kufuatia kipindi cha msimu mkungu kutoka kwa mkulima uuzwa kati 5000 hadi 10000 kama walivyokutwa katika Tarafa ya Kamachumu Wilaya Muleba mkoani Kagera juzi.*

## Habari

# 383,500 wafungiwa mita janja nchi nzima

**Na Mwandishi WETU**

IKIWA imetimia miezi minane tangu Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kuzindua mita janja za umeme, tayari jumla ya wateja 383,500 wamepata huduma hiyo nchi nzima.

Lengo la mita hizo ni kumwezesha mtumiaji anaponunua umeme kuingia moja kwa moja, tofauti na sasa ambapo baada ya kununua umeme unalazimika kuingiza tokeni kwenye mita au kwa kutumia rimoti.

Mita hizo za kielektroniki zina uwezo wa kuwasiliana kimfumo, hivyo kumwezesha mteja kulipia na kuingiza umeme kwenye mita moja kwa moja kama ilivyo kwenye ving'amuzi.

Akizungumza na Pambazuko, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Huduma kwa Wateja wa Tanesco, Irene Gowelle amesema baada ya kufanyika uzinduzi wa mita hizo mwaka jana, utekelezaji ulianza nchi nzima kuanzia Februari mwaka huu.

"Tayari jumla ya wateja 383,500 wamefungiwa mita janja za umeme nchi nzima na tulianza kuwafungia tangu Februari mwaka huu na wengine wanaendelea kufungiwa," amesema Gowelle.

Mita hizo janja ilizinduliwa na Waziri wa Nishati, Degratius Ndejembi Desemba 5, 2025 kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Katika uzinduzi huo Ndejembi aliagiza shirika hilo kusambaza mita janja nchi nzima kwa kuzingatia usalama wa wananchi na wateja wapya wafungiwe mita hizo.

Pia aliwaonya wenye nia ovu kutaka kujifanya wao ndiyo wanauza mita hizo, akisema asitokee mtu wa nje ya Tanesco akajifanya ndiye muuzaji.

Akitoa faida za mita hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco, Lazaro Twange alisema mita hizo zina faida, ikiwemo kutunza kumbukumbu kwa muda mrefu na zina suluhisho endapo mteja akinunua umeme kwa bahati mbaya.



*Waziri wa Nishati, Degratius Ndejembi*

"Zina taarifa zote juu ya mwenendo wa umeme hivyo zitapunguza mawasiliano ya huduma kwa wateja. Zina mifumo ya kiusalama pia na kulinda udhibiti wa mapato,"alisema Twange.

Meneja wa Kitengo cha Mita Tanesco, Mhandisi Nyanda Busumabu aliwahi kunukuliwa akisema hakuna gharama za kubadilisha mita ya zamani ili kupata janja.

"Kwa sasa hakuna gharama ambayo mteja atatozwa, ni program inayokwenda kwa awamu ya maeneo, lengo ni kufika nchi nzima. Tutawafikia wateja kwa namna hiyo…"

"Wateja wapya wanaoomba wanafungiwa kulingana na maeneo hayo hayo hadi tuwamalize. Hii ni program inayotekelezwa hatua kwa hatua na mwisho tutafikia wateja wote…"

"Hata sisi tunatamani hata kesho tuamke watu wote wawe wamefungiwa lakini kwa sababu ya utendaji ulivyo lazima kwenda hatua kwa hatua."

Akizungumzia kuhusu watu wenye haraka ya kufungiwa mita hizo, amesema wanapaswa kuwasiliana na ofisi za maeneo husika kama Tanesco wilaya au mkoa.

# Nguvu ya umma au mwelekeo mpya wa siasa Tanzania?

**Na Mwandishi WETU**

MICHANGO ya hiari iliyoanzishwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kwa ajili ya kukusanya fedha za kugharamia kikao cha Baraza Kuu imegeuka kuwa zaidi ya kampeni ya kuchangisha fedha.

Michango hiyo imeibua mjadala mpana kuhusu siasa za ufadhili wa vyama, uhalali wa uungwaji mkono wa wananchi, uwajibikaji wa viongozi wa kisiasa na nafasi ya dola katika ushindani wa kisiasa.

Kwa siku kadhaa, viongozi wa Chadema wamekuwa wakihamasisha wanachama na wafuasi wao kuchangia kupitia mifumo ya kidijitali.

Mwitikio mkubwa uliojitokeza umeifanya kampeni hiyo kuwa na mafanikio makubwa na kuibua mijadala mikubwa ya kisiasa nchini.

Lakini kwa mujibu wa maoni ya wadau mbalimbali, mafanikio hayo yamezua tafsiri mbili zinazokinzana.

Baadhi ya watu wanaona michango hiyo kama ishara kwamba Chadema bado kina mizizi imara kwa wananchi, licha ya changamoto mbalimbali za kisiasa ambazo kimepitia katika miaka ya karibuni.

Wanasema kuwa mwitikio ulioonyeshwa na wananchi unathibitisha kauli mbiu ya Chadema ya miaka mingi - nguvu ya umma.

Hii inatokana na sababu kuwa wananchi hawatoi fedha kwa sababu ya kulazimishwa, bali kwa sababu wanaamini chama hicho kinawakilisha matarajio yao ya kisiasa.

Hali hiyo imejionyesha kupitia kijana mmoja mkazi wa Arusha ambaye kupitia mitandao ya kijamii anasema haoni tatizo lolote kwa wao kukichangia chama hicho.

Kijana huyo ambaye hakutaja jina lake amekwenda mbali zaidi na kubainisha kuwa taarifa za ubadhirifu wa fedha zilizotolewa



*Makamu Mwenyekiti Chadema, John Heche*

kwa makamu mwenyekiti wa chama hicho, John Heche, haziwezi kuwa kikwazo kwa watu kuchangia.

Akasema yeye yupo tayari hata kumchangia Heche binafsi.

"(Heche) alete namba tutachanga. Hata kama akitaka kwenda kujenga ghorofa, sisi tutachanga tu," alisema.

Alipoulizwa nini kinampa utayari wa kuchangua, alijibu; "Yeye ndiye mtu pekee ambaye licha ya misukosuko yote ya kisiasa nchini amejitolea kutusaidia sisi wananchi wa kawaida, kama yeye amejitoa kwa ajili yetu kwa nini sisi tusijitoe kwa ajili yake?"

Lakini upande mwingine mwamko huo wa uchangiaji unaibua maswali ya msingi kuhusu uwajibikaji.

Wakosoaji wanahoji kwa nini viongozi wanawataka wananchi wakichangie chama wakati kuna tuhuma za matumizi mabaya ya ruzuku na fedha nyingine zilizochangwa kwa ajili ya chama.

Inaendelea Uk. 36

# Mtazamo


Gerson Msigwa

## Nguvu ya umma...

Inatoka Uk. 35

Hivi sasa chama hicho kipo kwenye mgogoro mkubwa uliokigawa baada ya baadhi ya wanachama kuibuka na kumtuhumu Heche kuwa alipokea fedha zilizochangwa kwa ajili ya chama lakini yeye akazitumia kwa matumizi binafsi.

Kwa wakosoaji hao, kabla chama hakijaomba michango mipya, chama kinapaswa kwanza kujenga upya imani kuhusu usimamizi wa fedha zilizowahi kuchangwa siku za nyuma.

**Mtihani wa kisiasa**

Kwa vyama vya siasa duniani, michango ya wanachama ndiyo kipimo muhimu cha afya ya chama.

Wachambuzi wa masuala ya siasa wanabainisha kuwa chama kinachoweza kugharamia shughuli zake kupitia wanachama wake huwa na uhuru mkubwa wa kisiasa kuliko kinachotegemea wafadhili wachache au ruzuku pekee.

Katika mazingira ya Tanzania, ambapo ruzuku za vyama zimekuwa sehemu muhimu ya uendeshaji wa shughuli za kisiasa, uwezo wa chama kukusanya fedha moja kwa moja kutoka kwa wananchi unaweza kutafsiriwa kama mtaji wa kisiasa.

Ndiyo hoja ambayo Makamu Mwenyekiti wa Chadema, John Heche, anaijenga anapolizungumzia suala hilo la mwamko wa wananchi kukichangia chama anachokiongoza.

Akizungumza hivi karibuni, Heche alisema chama kinashuhudia mwitikio mkubwa wa wananchi kiasi kwamba baadhi ya wapinzani wake wameingiwa na hofu.

Kwa mujibu wa Heche, kuna taarifa kwamba serikali inaweza kutafuta njia za kudhibiti michango hiyo kwa kuifanya ionekane kuwa ni marufuku kwa vyama vyote vya siasa.

Alidai hatua hiyo ingekuwa mbinu ya kuzuia Chadema bila kuonekana kukilenga moja kwa moja.

"Taarifa tulizonazo ni kwamba wanataka kufungia michango, lakini kwa sababu wakifanya hivyo itaonekana wanailenga Chadema, wamewatuma wengine nao waanze kuomba michango ili baadaye wakifungia ionekane vyama vyote vimefungiwa," alisema Heche.

Kauli hiyo imeongeza mjadala kuhusu mipaka ya mamlaka ya dola katika kusimamia shughuli za kisiasa na haki ya vyama kukusanya fedha kutoka kwa wanachama wake.

**Serikali yajibu hoja**

Wakati Chadema ikisisitiza michango kama ishara ya mshikamano wa kisiasa, serikali imechagua kujibu hoja hiyo kwa mtazamo wa uchumi.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, amesema badala ya viongozi wa kisiasa kuwahamasisha vijana kutoa fedha kwa vyama, wanapaswa kuwahamasisha kuzalisha mali.

Kwa mujibu wake, serikali imewekeza katika kujenga mazingira ya biashara, masoko na ajira ambayo yanapaswa kuwapa vijana kipato.

"Badala ya kuwahamasisha vijana kwenda kufanya shughuli za uchumi, wanawahamasisha watoe hela walizonazo wawapatie wao," alisema Msigwa katika ziara aliyoifanya kwenye maeneo kadhaa jijini Dodoma wiki iliyopita.

Alitumia mfano wa Soko la Wamachinga la Dodoma, akisema badala ya wafanyabiashara 2,700 waliotarajiwa, soko hilo sasa lina wafanyabiashara zaidi ya 4,800, huku mapato ya wengi yakiongezeka.

Alisema kwa mtazamo wa serikali, fedha ambazo wananchi wanachangia kwenye siasa zingekuwa na tija zaidi kama zingewekezwa kwenye shughuli za uzalishaji.

Inaendelea Uk. 37

# Nguvu ya umma...

Inatoka Uk. 36

**Hoja mbili zenye uzito**

Kwa wachambuzi wa siasa, hoja zote mbili zina uzito wake.

Kwa upande wa Chadema, uwezo wa kukusanya fedha kutoka kwa wananchi unaweza kuashiria kuwa chama bado kina mtandao mpana wa wafuasi wanaokiamini.

Katika demokrasia nyingi zilizoendelea, vyama vinavyojitegemea kifedha kupitia wanachama huonekana kuwa na uhalali mkubwa wa kisiasa.

Wachambuzi wanasema kuwa hilo linaonesha nguvu ya umma ambacho chama husika kinazo.

Lakini hilo pekee halitoshi.

Wachambuzi wanabainisha kuwa nguvu ya kukusanya fedha lazima iambatane na uwazi wa matumizi yake.

"Wanachama wanaochangia wanatarajia kuona taarifa za mapato, matumizi na mifumo madhubuti ya uwajibikaji," anasema mmoja wa wachambuzi wa siasa ambaye hakupenda kutajwa jina lake.

Wanadai kuwa kutofanya hivyo kunaweza kuibua maswali yale yale ambayo yamekuwa yakitolewa kuhusu usimamizi wa fedha ndani ya vyama vya siasa.

Hata hivyo, kwa miaksa kadhaa sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) hajawahi kuikuta Chadema na matatizo makubwa katika utunzaji wa hesabu zake kupitia ukaguzi anaoufanya kila mwaka.

Kwa upande wa Serikali, msisitizo wa kuelekeza nguvu kwenye uzalishaji wa uchumi unaendana na agenda ya kukuza kipato cha wananchi.

Hata hivyo, wachambuzi wanasisitiza kuwa hoja hiyo haiwezi kufuta haki ya wananchi kuchagua matumizi ya fedha zao, iwe ni kuwekeza kwenye biashara au kuchangia chama cha siasa wanachokiamini.

"Katika jamii ya kidemokrasia, uhuru wa kuchangia chama cha siasa ni sehemu ya uhuru wa kushiriki katika mchakato wa kisiasa, mradi shughuli hizo zinafanyika kwa mujibu wa sheria," anasema mchambuzi huyo.

**'Siasa za fedha' hatua mpya**

Mwamko huu ambao wanachama wa Chadema kukichangia chama chao wanaouonyesha katika miaka ya hivi karibuni ni jambo ambalo linatoa taswira mpya ya siasa za Tanzania.

Wachambuzi wanabainisha kuwa Tanzania inaingia katika kipindi ambacho ushindani wa kisiasa hautapimwa tena kwa mikutano na maandamano pekee, bali uwezo wa vyama kujenga uaminifu wa kifedha kwa wanachama wake.

Chama kinachoweza kuwashawishi wananchi kutoa fedha zao kwa hiari kinaonyesha kiwango fulani cha imani ya kisiasa, lakini imani hiyo lazima ilindwe kwa uwajibikaji wa hali ya juu, wanaonya wachambuzi hao.

Kwa Chadema, kampeni ya michango inaweza kuwa ushahidi wa uhai wa kisiasa na uwezo wake wa kuhamasisha wananchi.

Kwa serikali, mjadala huo umefungua nafasi ya kusisitiza ajenda ya uzalishaji, ajira na ukuaji wa uchumi.

Hatimaye, mjadala huu hauhusu fedha pekee. Unahusu swali kubwa zaidi; katika mazingira ya ushindani wa kisiasa wa Tanzania, je, nguvu ya chama inapimwa kwa idadi ya watu wanaohudhuria mikutano yake, au kwa idadi ya wananchi walio tayari kutoa fedha zao kukiunga mkono?

Jibu la swali hilo linaweza kuwa moja ya viashiria muhimu vya mwelekeo wa siasa za Tanzania kuelekea uchaguzi mkuu ujao.



## Makala Kimataifa

# AI yatumika kusaidia magaidi kushambulia



Na Mwandishi WETU

MAENDELEO ya sayansi na teknolojia hayawasaidii tu watu wenye nia njema, hata magaidi nao wameanza kunufaika na maendeleo hayo.

Taarifa zinaeleza kuwa makundi kadhaa ya kigaidi kama vile Boko Haram, yameanza kutumia teknolojia ya akili mnemba au Artificial Intelligence (AI) kupanga na kutekeleza mipango yao haramu.

Taarifa ya utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Cambridge nchini Uingereza zinaeleza kuwa vikundi hivyo vimeanza kutumia teknolojia ya kisasa kupanga mipango ya kushambulia.

Hayo yalibainika wakati wa utafiti ambao ulihusisha mahojiano ya kina na wanachama wa zamani wa kundi la kigaidi la Boko Haram la nchini Nigeria.

Katika mahojiano hayo, wanachama hao wastaafu walieleza jinsi kundi hilo la kigaidi linavyotumia AI kuimarisha uwezo wake wa kufanya mashambulizi tangu mwaka 2023.

Wataalamu waliochambua utafiti huo wanasema kuna uwezekano siyo Boko Haram peke yake wanaofanya hivyo, bali na makundi mengine ya kigaidi.

Taarifa zilizopatikana zinaeleza kuwa kundi hilo linaamini kuwa kama Mungu amewasaidia katika shughuli zao, basi hata AI nayo inaweza kuwasaidia.

Utafiti huo ulihusisha mahojiano na zaidi ya wanachama 20 wa Boko Haram ambao hivi sasa wameachana na kundi hilo.

"Kwa kawaida ni vigumu sana kuwapata watu wa aina hii kuzungumzia suala hili kwa uwazi," anasema Antonia Juelich, mtaalamu wa masuala ya teknolojia na ugaidi na mwandishi wa ripoti hiyo.

"Kitu ambacho kimerahisisha kazi ni kuwa nimekuwa nikiifanya kwa takribani muongo mmoja hivi sasa, inahitaji kujenga uaminifu mkubwa ili kuwapata watu watakaozungumzia suala hili kwa uwazi," anasema.

### Mabadiliko

Hadi siku za hivi karibuni taarifa zilionyesha kuwa matumizi ya teknolojia za kisasa miongoni mwa makundi ya kigaidi yalionekana kupitia nyayo zao walizoziacha katika intaneti.

Iliaminika kuwa kwa kiasi kikubwa makundi hayo yalikuwa yakitumia mitandao ya kijamii kama vile telegram kwa ajili ya kufanya propaganda na kusambaza habari za uongo, kurubuni au kutafuta wanachama wapya.

Lakini Graig Klein, mtaalamu wa ugaidi wa kimataifa anayefanya kazi Chuo Kikuu cha Leiden, Uholanzi ambaye pia amewahi kufanya utafiti wa matumizi ya AI miongoni mwa vikundi vya ugaidi, anabainisha kuwa mahojiano hayo yanaunga mkono kile alichokibaini katika utafiti wake.

Mahojiano ya karibu zaidi yalifanyika katikati ya mwaka jana.

Kwa mujibu wa utafiti huu mpya, Kundi la Boko Haram lilianza kutumia AI mwaka 2023, miezi michache tu baada ya kuzinduliwa kwa ChatGPT mnamo Novemba 2022.

"Hakuna jambo ambalo tuliliuliza kupitia mtandao huo ambalo hatukupata majibu yake. Tunaamini kuwa (ChatGPT) inajua kila kitu," alisema mmoja wa waliohojiwa.

Anasema kuwa wataalamu kutoka Iraq, Afghanistan, Afrika kaskazini na nchi nyingine

Inaendelea Uk. 39

# AI yatumika kusaidia

Inatoka Uk. 38

waliwafundisha jinsi ya kuitumia ChatGPT hasa jinsi ya kuuliza maswali ili kupata jibu lenye usahihi zaidi.

Alisema kuwa moja na mbinu walizofundishwa ilikuwa inajulikana kama "kuvunja gereza" inayohusisha maarifa ya kuuliza swali huku ukikwepa vikwazo vyote vya kimaadili ambavyo vimewekwa ndani ya program nyingi za AI.

Anasema vikwazo hivyo mara nyingi vinaizuia AI kutoa majibu yenye ufasaha, hasa kwenye masuala ambayo si ya kimaadili.

Kwamba walikuwa wanauliza vitu kama vile jinsi ya kutengeneza mabomu ya aina mbalimbali na kutokana na ujuzi wa kuuliza walikuwa wanapata majibu mujarabu.

Baada ya matumizi ya teknolojia hii kushamiri matawi kadhaa ya Boko Haram wakatengeneza idara ndogo ndani yake zinazohusika na matumizi ya AI katika makundi yao na kuwa baada ya kuwa na usajili wa AI kwa haraka waliweza kuwapatia wapiganaji wao taarifa zote muhimu walizozihitaji.

Katika baadhi ya matukio, walikuwa wanaulizia kuhusu matumizi ya silaha mpya ambazo waliziteka katika mapigano – hasa zile ambazo hawakuwa na utaalamu nazo.

Pia kwa kutumia AI waliweza kupanga mashambulizi yakilenga kukwepa mitego inayowekwa na wale wanaokabiliana nao.

Juelich anasema AI ilikuwa ikitumiwa na makundi haya siyo kwa ajili ya propaganda pekee, bali kupanga na kuratibu mpango mzima wa mashambulizi.

Klein alibainisha kuwa program kadhaa za AI ambazo zilitengenezwa na watalaamu kwa ajili ya kuwasaidia watu duniani zimegeuka kuwa hatari kwani sasa zinatumiwa na magaidi kurahisisha mambo yao.

"Program hizi zina uwezo wa kuyafanya makundi haya kuwa hatari zaidi kwa sababu zinaviwezesha vikundi hivi kuimarisha ufundi wao na kuifanya mikakati yao kuwa mizuri zaidi kuliko njia za kawaida zilizozoeleka," anasema.

Akithibitisha hilo katika mahojiano, mmoja wa waliohojiwa aliyekuwa akilitumikia kundi la Islamic State West Africa Province (ISWAP) – ambalo ni tawi la Boko Haram alisema: "Tuliwapeleka wapiganaji 200 kwa sababu tulikuwa na wapiganaji wengi, lakini 60 wakauawa na kwa kutumia AI, tukajifunza kuwa wakati mwingine inakuwa vizuri zaidi kupeleka wapiganaji 20 tu…"

"Tulijifunza jinsi ya kupanga mashambulizi yenye ufanisi mkubwa kwa kutumia watu wachache."

AI pia imeyasaidia makundi haya kupata masuluhisho ya jinsi makundi hayo yanavyoweza kukabiliana na changamoto mpya.

Mathalan, mmoja wa waliohojiwa anasema, wakati wanajeshi wa Nigeria walipoanza kuchimba mifereji kuzunguka kambi zao ili kuwazuia wasitumie pikipiki ambayo ndio ilikuwa njia yao kuu ya kufanya mashambulizi, ilikuwa ni chatbot ambayo iliwafundisha njia mpya ya mapambano na jinsi ya kuruka na pikipiki kwenye mifereji hiyo.

"Kitu ambacho AI inatuwezesha kufanya kwa usahihi ni kujaribu na kukosea bila ya kukifanya kitu hicho kwa uhalisia," anasema.

"Hata kama tukipata taarifa mpya ambazo hatuzifahamu kwa undani tulikuwa na uwezo wa kupata mchanganuo wake haraka sana kwa kuuliza kwenye ChatGPT."

Anasema kutokana na utandawazi ni dhahiri kuwa Boko Haram siyo kikundi pekee cha kigaidi ambacho kinatumia teknolojia hiyo kuimarisha shughuli zake.

### Kutengeneza mabomu

Klein anasema kupitia AI, makundi haya yanapata taarifa zote za jinsi ya kutengeneza mabomu lakini kinachokwamisha kufanya hivyo ni upatikanaji wa vifaa vinavyohitaji.

Anasema kwa kutumia mbimu ya "kuvunja gereza" wanaweza kuuliza ChatGPT na kupata taarifa hizo kirahisi.

Na Anti MSHAURI





# Ushirika kwa wanandoa

NAKUSALIMU msomaji wangu wa safu ya uhusiano. Karibu uweze kujifunza masuala mbalimbali ya maisha.

Wiki hii nitazungumzia misingi ya wanandoa kusaidiana kutekeleza majukumu ya familia na hata jamii na ndugu.

Katika maisha ya familia, mwanaume ndiye anabeba majukumu makuu ya familia na ndiye anayetarajiwa kutafuta riziki, kulinda, na kuongoza nyumba. Hili ni jukumu zito linalostahili kupongezwa na kuthaminiwa.

Hata hivyo, kuwa mbeba majukumu haimaanishi kwamba mwanamke anapaswa kukaa kimya na kutazama tu.

Ndoa ni ushirikiano na safari ya watu wawili. Hivyo mke naye ana mchango wake, awe anafanya kazi ama biashara au hata kuwa mama wa nyumbani.

Tukumbuke kuwa mkono mmoja hausagi na kichwa kimoja hakiendi mbali, bali mzigo ukigawanyika huwa mwepesi.

Mwanaume anapoleta kipato na mwanamke akisaidia kupanga matumizi, kutunza nyumba, na kutoa ushauri, familia inapata utulivu na kwenda kwa utaratibu mzuri.

Neno la kumtia moyo, maombi, na amani nyumbani vinampa mwanaume nguvu ya ziada ya kurudi kazini na kupambana kwa bidii zaidi kwa ajili ya familia yake. Pia, wanandoa wakiwa timu moja ndoa huimarika.

Changamoto kama ugonjwa, kupoteza kazi, au gharama za shule zinapojitokeza, familia isiyo na ushirikiano huanguka kwa urahisi.

Lakini wale wanaosaidiana husimama pamoja, wanafikiria pamoja na kupata ufumbuzi na hali hiyo huwafanya watoto kujifunza mengi kutoka kwa wazazi wao.

Wakiona mama na baba wanashirikiana katika kazi za nyumbani na kufikia uamuzi, wanajifunza upendo, heshima, uvumilivu na umuhimu wa kazi ya pamoja.

Hali hii inajenga vizazi vijavyo vyenye misingi imara na maadili. Muhimu zaidi, msaada wa mwanamke haupunguzi uongozi wa mwanaume bali unazidisha na kuufanya uwe rahisi.

Kiongozi aliye na timu nyuma yake hufika mbali zaidi kuliko anayepambana peke yake. Tubadili mtazamo; mwanaume abebe majukumu yake kwa ujasiri, na mwanamke amshike mkono kwa upendo na hekima. kwa sababu nyumba hujengwa na watu wawili, sio mmoja.

Tukumbuke kuwa ndoa yenye ushirikiano ndiyo msingi wa jamii yenye mafanikio amani na maendeleo.

Tukutane wiki ijayo.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***

# Mbinu za kupendeza bila gharama kubwa

WATU wengi huona kuwa kununua nguo ya gharama kubwa ama kutumia pesa nyingi kushona nguo ndiyo huwafanya kupendeza suala ambalo si kweli.

Suala la kupendeza ni namna unavyoweza kupangilia mavazi yako kwa mfuatano wa rangi husika.

Leo katika safu hii nakugusia kuhusu rangi nyeusi na nyeupe namna ambavyo zitakupa muonekano chanya.

Gauni la rangi nyeupe unaweza kulivaa kwa koti la rangi nyeusi, pinki ama kijani na ukapata mwonekano wa gharama hata kama umenunua nguo za bei rahisi.

Gauni jeusi unaweza kulivaa na koti la rangi nyeupe, light blue au pinki.

Katika mavazi haya, vaa viatu virefu vya rangi nyeusi vya kufunika. Beba pochi ya rangi nyeusi ili kukamilisha vazi lako.

Vazi hili unaweza kulivaa ofisini na likakupa muonekano wa gharama kubwa.



# Unavyoweza kurefusha kope zako

KOPE ni moja ya sehemu muhimu katika sura ya binadamu ambayo pamoja na sababu za kisayansi kuwepo hapo, kuna zile za kiurembo pia.

Kope hupendeza zaidi zikiwa ndefu hivyo huwalazimu baadhi ya wanawake kuzichana kwa mascara, ili kuziweka katika hali ya kunyooka na kuvutia huku wengine wakibandika ambazo ni bandia.

Pamoja na mbinu hiyo, leo nimekuandalia namna bora ya kurefusha kope pasipo madhara.

Mbinu hiyo ni kutumia mafuta ya mgando ya Vaseline.

Katika kukuza na kujaza kope pakaa Vaseline kwenye kope zako kila siku usiku kabla ya kulala. Kwenye zoezi hilo, utaona mabadiliko baada ya wiki mbili hadi tatu.







# Lavalava ajengea wazazi wake nyumba ya kifahari

Na Mwandishi WETU

MSANII wa Bongo Fleva, Lava Lava, ametangaza kuwajengea wazazi wake jumba la kifahari, akisema ametimiza ndoto aliyokuwa nayo kwa muda mrefu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Lava Lava amesema anamshukuru Mungu kwa kufanikisha hatua hiyo, huku akikumbuka maisha magumu waliyowahi kupitia kabla ya mafanikio.

"Tulitoka mbali, tumepitia mengi lakini hatukuchoka kupambana. Alhamdulillah, leo nimetimiza ndoto ya kuwajengea wazazi wangu," ameandika Lava Lava.



# Kajala alimvyomshukuru Lamata kumzawadia kiwanja

Na Mwandishi WETU

MTAYARISHAJI na mwongazaji wa filamu nchini, Lamata Leah, amemzawadia kiwanja rafiki yake, Kajala, kwenye siku yake ya kuzaliwa.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Kajala amesema Lamata alianza kama rafiki, lakini sasa amekuwa sehemu ya familia yake, huku akimpongeza kwa moyo wake wa upendo, ukarimu na kujali.

"Kuna watu Mungu huwaleta kwenye maisha yetu kama marafiki, lakini mwisho wake wanakuwa familia. Wewe ni mmoja wao. Asante kwa kuniongezea asset nyingine.

"Ulichonifanyia kimenigusa kwa namna ambayo siwezi kuelezea kwa maneno. Kuninunulia kiwanja ni zawadi ambayo si kila mtu anaweza kutoa na imenionyesha jinsi ulivyo na moyo wa upendo, ukarimu na kujali. Nakupenda sana, Mungu akutunze kwa ajili yangu," ameandika Kajala.

Na John Marwa





# Hasta luego Copa del Mundo Fifa 2030

WAHISPANYOLA kwa wino mzito wametufungia mzunguko wa 23 wa Fainali za Kombe la Dunia 2026 kwa kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Hispania walitawazwa kuwa mabingwa wapya wa kombe hilo Julai 19 katika Dimba la Metlife lililoko mashariki mwa Rutherford, New Jersey, Marekani.

Kutoka mataifa 48, michezo 104, huku mpira wa kitaalamu wa 'Trionda' ukitumika, Hispania wamedhihirisha wao ni wababe wa soka duniani baada ya kuwahenyesha mabingwa watetezi Argentina - ambayo ilikuwa na hazina ya Lionel Messi, kwa bao 1-0.

Hispania inatwaa ubingwa wao wa pili mara baada ya kufanya hivyo miaka 16 iliyopita katika ardhi ya Nelson Mandela pale Afrika Kusini 2010, walipowaacha Waholanzi na majonzi.

Timu hiyo ya Hispania imeweka historia kwa kuchukua taji hilo pasipo kupoteza mchezo wowote kuanzia hatua ya makundi hadi fainali.

Rekodi mpya ya mfungaji bora imewekwa katika michuano hiyo baada ya Kylian Mbappe wa Ufaransa, ambaye amefikisha mabao 22. Alifunga mabao 10 katika michuano hiyo pekee.

Fainali hizo – kwa mara ya kwanza ziliandaliwa na mataifa matatu; Marekani, Canada na Mexico, ambapo imethibitika kuwezekana kwa mataifa zaidi kuandaa mashindano hayo.

Katika michuano hiyo, Timu ya Taifa ya Cape Verde iliweka historia kwa kuwa ya kwanza kutoka Afrika kushiriki kwa mara ya kwanza na kutopoteza mchezo ndani ya dakika 90, michezo mitatu ya hatua ya makundi na mchezo mmoja wa 32 bora hawakupoteza katika muda wa kawaida wa kucheza.

Mlinda mlango wa timu hiyo, Vozinha (41) alikuwa kivutio kwa wapenzi na wahafidhina wa kandanda ulimwengu kwa kuonyesha kiwango bora cha kuzuia mabao ya wazi hata mahali ambapo ilionekana kutowezekana.

Lakini yapo uliyoyaona wewe pia, Wahispanyola wanasema; "Hasta luego Trionda, hasta luego Copa del Mundo Fifa 2030" – yaani; "Tutaonana tena, Trionda; tutaonana tena, Kombe la Dunia la Fifa 2030.



# Mtori wa usajili una nyama?



Cherki Toure

Na John MARWA

WAKATI maandalizi ya kuelekea msimu mpya wa kandanda 2026/27 yakiwa yameshika kasi, miongoni mwa habari kubwa zinazotikisa, ni usajili wa wawakilishi wa Tanzania katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika; Simba, Yanga, Azam FC na Singida Black Stars.

Huu ndio wakati unaotoa tafsiri ya uimara, ubora na uhalisia wa kile ambacho klabu inaenda kukifanya katika msimu mzima kupitia usajili mpya.

Kuwepo kwa wachezaji wapya wanaokuja kuongeza nguvu na kuimarisha vikosi na mpango kazi unaobebwa na utimamu wa mwili na akili kwenye mkoba wa mbinu za mwalimu, matokeo yake ndiyo yanayosubiriwa kwa hamu kubwa.

Lakini je, usajili unaofanyika unakuwa na taji ndani ya kiwanja kulingana na ukubwa wa mashindano ambayo klabu zinashiriki kwa msimu husika? Kumekuwa na utamaduni wa klabu zetu kufanya usajili unaobamba mitandaoni kwa mapambo ya wasifu usiosanifu ubora dimbani.

Misimu kadhaa hivi karibuni klabu hizo zimekuwa kama daladala ambazo hupakia kila msafiri, na wengine wakiwa ni abiria wanaosubiri kituo cha msaada kushuka kabla ya kulipa nauli.

Kila timu na mashabiki wake wanatamba kwa usajili murua kwa "kushusha." Simba wakitamba kwa kuwapata nyota Ibraheem Jabaar, Keletso Makgalwa, Ibrahim Doumbia, Kelvin Nashon, Bakari Msimu na Nathaniel Chilambo.

Huko Jangwani nako, Yanga ikijishaua kwa kupata Saini za Ibrahima Toure, Albert Kangwanda, Housseine Zakouani, Erick Mwijage, Mohamed Mussa, Abdulnasir Muhamed, Hussein Mihambo, Issa Abushiri.

Matajiri wa Jiji – Azam, nao wameanika silaha mpya wakiwemo Caleb Ilese, Taiwo Abdulrafiu, Donovan Makoma, John Mano, Hassan Mubiru, Henoc Molia, Lupini Dieumerci Henri Stanic pamoja na urejeo wa Kipre Junior.

Ukitazama usajili huo kwenye dirisha kubwa ni maingizo ya wachezaji zaidi ya saba kwa kila timu, kila msimu na kila dirisha la usajili, je, usajili huo unaenda kutibu udhaifu uliojitokeza msimu uliopita hasa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho?

Majibu ya maswali hayo ni kusubiri matokeo ya uwanjani, na kuona endapo wachezaji hao na walimu wao wanaleta kile kinachotamaniwa na wadau wote wa soka.

Dakika ndani ya uwanja na kupulizwa kwa kipyenga kutabainisha uwezo na ari ya kila timu kutetea ukuu wake.

Hapo ndipo wapenzi wa soka watabaini kuwemo kwa finyango za nyama kwenye mtori au vinginevyo.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION